# MABWANA, SISI TUNATAKA KUMWONA YESU

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru, usiku wa leo, kwa ajili ya ahadi tulizo nazo katika wimbo huu. Tunaweza tu kumwona mvulana mwenye kifafa katika mshtuko ule, baba yake akija kukutana na Wewe, na kuomba kama ungemrehemu. Naye akasema, "Ninaweza kama ukiamini. Mambo yote yanawezekana kwao waaminio."

3 Uliahidi ya kwamba kamwe hutatuacha wala kutupungukia. Maandiko yanasema Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe uko tayari tu, usiku wa leo, kuponya magonjwa yetu kadiri ulivyokuwa wakati huo, kwa kuwa Wewe ni yeye yule. Nawe uliahidi katika Neno Lako ya kwamba mambo uliyofanya, sisi pia tungeyafanya. Hiyo ni ahadi Yako, nasi tunajua ya kwamba ni ya kweli.

4 Kwa hiyo naomba ahadi hizi zote kuu, Bwana, zitimizwe kwa watoto Wako usiku wa leo, ili kila mtu apokee kile alichokujia. Na wakati ibada itakapofungwa jioni ya leo, nasi tuende kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tusemezane miongoni mwetu kama wale waliotoka Emau siku ile. Ulikuwa umetembea pamoja nao siku nzima, nao hawakukujua. Lakini usiku huo, wakati ulipowaketisha peke yao chumbani, Wewe ulifanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya kule kusulubiwa, jambo ambalo hakuna mtu mwingine aliyelifanya vivyo hivyo hasa. Ndipo wakatambua kwa *hili* ulilofanya, ya kwamba Wewe ulikuwa Kristo aliyefufuka. Nao wakasema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?"

5 Tunaomba ya kwamba Wewe utarudi kwetu, usiku wa leo, Bwana. Watu hawa wachache tu, bali Wewe ulisema, "Wawili au watatu wakikusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Hiyo ni ahadi Yako, Bwana, nasi tunaamini kwamba ni kweli. Tunangojea sasa, katika Jina la Bwana Yesu, kwa ajili ya kuthibitishwa kwa Neno Lako. Amina.

Mnaweza kuketi.

[Ndugu fulani anatoa unabii—Mh.]

6 Amina. Shukrani ziwe kwa Baba yetu wa Mbinguni kwa himizo hilo kuu. Jinsi linavyopaswa kutufanya tujisikie, kabla ibada haijaanza, Yeye ametupa ahadi kwa roho ya unabii, kwamba tutamwona Yeye miongoni mwetu hapa ndani. Sasa, ndivyo ilivyo? Bila shaka ndivyo ilivyo. Unatoka kwa Mungu.

Chochote kinachotoka kwa Mungu daima ni sahihi. Jina la Bwana libarikiwe.

7 Ninashukuru sana kuishi katika wakati ambapo Roho wa Mungu yuko katikati ya watu Wake, akiita, akilitenganisha Kanisa apate kulipeleka Nyumbani kwa ajili ya masalia watakaosalia duniani wakati atakapokuja, wapate kupokelewa juu Mbinguni. Ninashukuru sana kwa ajili yake.

8 Loo, hii ni saa kuu. Nina—nina furaha sana kuishi hapa. Mnajua, Musa angalipenda kuishi katika wakati huu. Mitume wote wangetaka kuwa wakiishi katika wakati huu. Na sisi hapa, tukiishi katika wakati huu, na tumepungukia katika majaliwa yetu. Jinsi ambavyo Mungu anataka kuwabariki watu Wake.

9 Sasa, mwajua, tunaambiwa ya kwamba siku ile Bwana atakapokuja, ingekuwa kwa namna fulani isiyotarajiwa, nalo kanisa lingekuwa linapoa. Nami ndiyo kwanza nimalizie, maskanini mwangu nyumbani, na zile—zile nyakati saba za mwisho za kanisa. Nazo zinatolewa. . . ziko kwenye kanda sasa, na ni, nilichukua kila wakati wa kanisa, kila usiku, nikafanya *Nyakati Saba Za Kanisa*, zile saba za mwisho. . . vile vinara vya taa, na wale wajumbe saba wa nyakati za kanisa na. . .

10 Mimi, kwa wote. . . Mimi ni mhubiri duni, lakini yote ambayo mimi. . . kila jitihada niliyowahi kutoa kwa ajili ya Bwana maishani mwangu mwote, siamini ilipata kuwa na ufanisi kama huo.

11 Kwa kuwa mara niliposhuka, na bila kujua jinsi ya kuchora nyakati hizi za kanisa ubaoni, nikionyesha ni kiasi gani cha Roho Mtakatifu kilichokuja katika Wakati wa Kanisa la Efeso, kisha kuendelea mpaka Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na kuendelea, na kama Malaika huyo wa Bwana, Nuru hiyo, haikuja moja kwa moja mbele ya watu mia tatu, ikajisogeza Yenyewe moja kwa moja ukutani, na kuchora kwa Nuru hiyo ya mviringo, jinsi tu nilivyoyachora hayo makanisa, na kuonyesha vilindi vile vile na kila kitu, wakati ikipita, huku watu mia tatu wakipiga mayowe, na kulia, na kuiangalia kando ya ukuta! Mbona, ilisimama hapa nje, na kujiakisi Yenyewe ukutani na kufanya kitu kile kile.

12 Nao wameichora sasa, katika picha, nayo imesimama maskanini. Bw. Arganbright, ndugu yetu mpendwa wa thamani, ndio kwanza atoke pale juu, na kwenda kuiangalia, mahali ilipokuwa ukutani.

13 Tunaishi tu katika wakati wa ajabu sana. Lakini ninahofia kwamba hatuninii. . . inatubidi kujibinya kidogo na kujitikisa kidogo tupate kujua mahali tulipo.

14 Mara nyingi nimesema, na kutoa tamshi hili: Mimi huona matabaka mawili ya watu ninaposafiri ulimwenguni, hayo ni moja la Kipentekoste, hilo lingine ni la kimsingi.

15 Sasa, watu wa kimsingi kimahali wanajua kile walicho katika Kristo kwa ahadi ya Biblia, bali hawajampokea Roho Mtakatifu kujua wao ni nani, ama, kuwa na imani. Sasa, Wapentekoste wamempokea Roho Mtakatifu, bali hawajui wao ni nani. Mnaona? Kwa hiyo ni kama tu mtu aliye na pesa kwenye benki, wala hajui jinsi ya kuandika hundi; huyo mwingine anaweza kuandika hundi, wala hana pesa kwenye benki.

16 Sasa, kama ungeweza kuwaleta hao wawili pamoja! Laiti Wapentekoste wangeweza kujituliza! Kama nilivyosema jana usiku (kweli ninaamini hili kwa moyo wangu wote.), kanisa la Kipentekoste lilikuwa katika hali bora zaidi . . . Si—sikuwa mhudumu siku hizo, wala sidhani nilikuwa, labda sikuwa duniani siku hizo. Lakini ile mikutano ya kale ya Mtaa wa Azusa ambayo mnazungumzia sana, nami nimesoma vitabu vyake, lile kanisa la mwanzoni la Kipentekoste, miaka thelathini ama arobaini huko nyuma, walikuwa katika hali nzuri zaidi kwa ajili ya kuja kwa Bwana kuliko walivyo sasa hivi. Kwa kweli walikuwa Wakristo kwelikweli, nao waliuishi. Waliuamini.

17 Sasa, *tumejipanga* wenyewe, nasi tuna mashirika yetu na madhehebu ambayo yanasimama katika tabaka. Nasi tuna wajukuu ambao wameingizwa ndani kwa kupewa mamlaka na kadhalika. Hatuna ule ukoo wa kale wa Wapentekoste ambao walikuwa wakifa na kupata ushindi kweli na Mungu, imani ile halisi ya kweli. Walimwomba Mungu tu, nao wakawapaka mafuta, kisha wakaenda wakaponywa.

Siku hizi Mungu anaweza kushuka na kujionyesha Mwenyewe kimiujiza, moja kwa moja miongoni mwa watu na kila kitu, na, kusema tu, "Vema, nadhani hilo lilikuwa ni zuri sana."

18 Mmekuwa na mafundisho mengi kupita kiasi, mkitafuta nuru mpya. Hicho ndicho Hawa alichokuwa akitafuta wakati macho yake yalipopofushwa. Mnaona, rudini tu kwenye Biblia na mdumu moja kwa moja na ule mtindo wa kale. Msiiache njia hiyo ya kale ya upendo wa kwanza, na jambo la kwanza linalowajia. Ishini na Roho Mtakatifu. Msiiendee hamaki nyingine. Dumuni moja kwa moja na Mungu, moja kwa moja katika Neno Lake. Naye Roho Mtakatifu kamwe hatakufanya ufanye jambo ambalo ni kinyume na Neno hili. Atadumu moja kwa moja katika Neno, maana Ne—Neno ni Mungu.

19 Jana usiku nilikuwa nikizungumza juu ya somo la *Matarajio*, halafu usiku wa leo, nilikuwa nikitaka kuwaombea wagonjwa. Sasa, katika sehemu ijayo, ifuatayo, kuanzia kesho usiku, tunataka kuanza kwenye Ujumbe wa kiinjilisti, labda *Kuja Kwa Bwana*, *Alama Ya Mnyama*, *Muhuri Ya Mungu*, *Wale Mia Na Arobaini Na Nne Elfu, Wale Wapanda Farasi Wanne Wa Ufunuo*. Mbona, ninaamini jumbe hizo ndizo tunazopaswa kuwapelekea watu, tupate kuwaamsha, kuwatikisa, kuwaonyesha ya kwamba

sisi...Nimeona matokeo makuu katika *Nyakati Saba Za Kanisa*. Ningepitia hizo tena, kama nilifikiri ingesaidia hapa. Jinsi ambavyo ninii...Mungu alizibariki.

20 Sasa, hebu niwaonye watu, tena na tena: Msitarajie mtikiso wa mwisho wa Mungu Kanisani kuwa ni jambo la ulimwengu mzima. Hautakuwa. Ni kwa Kanisa. Ni yale mambo makuu yatakayotendeka kwa watu walio katika uchache. Hilo ndilo kundi dogo ambalo Mungu analitikisa lijitayarishe, kuondoka. Hao wameondoka kwa vyovyote vile. Mnaona? Sasa, hilo ni la Kimaandiko na la Biblia.

21 Si muda mrefu uliopita mchungaji wa mji fulani mashuhuri alinijia, naye akasema, "Vema, ninazeeka." Kasema, "Nimekuwa hapa miaka ishirini na kitu, nasi tumekuwa na baadhi ya mikutano yenye nguvu sana." Ni Chicago, ni Mattsson-Boze.

22 Akasema, "Nimetamani, Ndugu Branham, na nikaja hapa na kupata unabii kutoka kwa Bwana kama ningekuja hapa, ningeuona mkono wenye nguvu wa Mungu ukitikisa mahali hapa kabla ya wakati wa kuondoka."

23 Nikasema, "Ndugu Joseph, kusema kweli," nilisema, "wewe ni mwanatheolojia mashuhuri, nawe ni mtu mashuhuri wa... Daktari wa Uungu. Hakuna shaka kuhusu hilo. Nisingeweza kuligusa." Lakini nikasema, "Lakini ndugu yangu mpendwa, una upambanuzi duni wa kiroho."

24 Hapo ndipo kanisa linapoikosea leo, ni huo upambanuzi wa kiroho kuona yale Mungu anayofanya. Nao wanaangalia mbali sana juu ya kitu hapa kinachoendelea papa hapa, nacho kitakupita kabla ya kukijua.

Hivi Yesu hakusema kuhusu Yohana...? Wanafunzi walisema, "Kwa nini waandishi wanasema ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?"

25 Akasema, "Tayari amekuja wala hawakumtambua." Jambo ndilo hilo. Kamwe hawakujua Eliya alikuwa ni nabii, kweli, ila Kanisa tu. Wasingalimtendea, wasingemwita "mzee kipara," na kupayuka-payuka namna hiyo. Hawakujua jambo hilo.

26 Hawakujua ya kwamba Yohana alikuwa kweli ni nabii wa Mungu. Walidhani alikuwa ni mwendawazimu huko nje nyikani, akijaribu kuwazamisha watu majini. Lakini kamwe hakuingia katika miji na kadhalika. Alikaa huko nje nyikani, asiye wa kawaida, wa kipekee. Nao walidhani alikuwa mlokole, jinsi alivyovalia. Lakini Kanisa, Kanisa lililoitwa, lililoitwa kuona jambo hilo, walitambua upesi sana ya kwamba yeye alikuwa ni nabii.

27 Hawakujua Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu mpaka alipokufa, akazikwa, na kufufuka tena. Wengi wao bado hawalijui hata wa leo. Ni kweli. Kamwe hawakujua, wao...

28 Kanisa Katoliki kamwe halikumkubali Mtakatifu Patrick. Shule zake zote zilikuwa huko Ayalandi ya Kaskazini. Aliwapinga maaskofu wa Katoliki, na sasa wanamtakatifuza. Mbona, kanisa Katoliki lilimchoma moto Joan wa Arc, huku akilia kwenye nguzo, kwa sababu walisema alikuwa ni mchawi. Huyo msichana aliona maono. Alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Yapata miaka mia moja baadaye walitambua hilo, akiisha kufa na kuzikwa. Kwa hiyo wakatubu, wakaichimbua miili ya hao makasisi waliomwua, wakaitupa mtoni.

29 Hawajui hilo kamwe mpaka limepita, naye Roho Mtakatifu analipa Kanisa wito wake wa mwisho sasa, na kufanya yale hasa Biblia ilisema lingefanya, nao Wapentekoste wanapapasapapasa juu yake, wakitazamia kitu fulani. Loo, jamani. Msifanye hivyo, tafadhali.

30 Sikilizeni. Kama tunamtarajia Kristo aje . . . Mnaamini hilo? Vema, tunamtarajia, hebu na tutende hivyo. Tunawezaje kumtarajia Kristo kuja, huku tukiweka dola milioni sita katika jengo? Mnapataje mambo haya makubwa mno, huku mkizungumza juu ya kuja kwa Kristo? Mbona, ndugu, inatupasa, kuwa tukijiandaa kwa ajili ya Unyakuo, si kwa ajili ya kukaa miaka mingine mia tano hapa duniani. Mnaona?

31 Kuna kasoro. Kwa namna fulani halina maana. Ha—halina maana kwangu mimi. Kwa matunda yao . . . Unaweza kulisema kwa midomo yako, lakini kwa moyo wako. Unaona?

Unasema, "Loo, naam, ninaamini Kristo yuaja." Lakini tendo lako linathibitisha vinginevyo.

32 Vipi kama mwanamume alimwambia mkewe anampenda kisha atoroke na mwanamke mwingine. Mnaona? Matendo hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno. Hiyo ni kweli. Haidhuru tunasema nini kwa midomo yetu, matendo yetu yanathibitisha kile kilicho moyoni mwetu. Hivyo ndivyo Yesu alivyosema, "Enyi wanafiki, mnawezaje kusema mambo mema? maana kinywa cha mtu hunena yaujazayo moyo." Mnaona? Na kama sivyo, basi ni unafiki. Kwa hiyo mnaona mahali ambapo Mungu angetuweka? Katika Wakati huo tu wa Kanisa la Laodikia, vuguvugu, akinena kutoka midomoni mwake, lakini moyo wake uko mbali sana.

33 Ee Mungu, hebu tugeuze kitu hicho nyuma. Hebu tumrudie Mungu. Hebu turudi kwenye Maandiko na tukae hapo mpaka tutakapoirudisha Pentekoste katika moyo wa mwanadamu, si kuirudisha katika madhehebu, bali kuirudisha katika moyo wa watu katika madhehebu. Mnaona? Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Kwa hiyo Mungu na atusaidie juma hili kufanya hivyo.

Ninaomba, ninafunga, ninamngojea Mungu. Ninataka kufanya sehemu yangu wakati nikiwa hapa California. Wewe fanya sehemu yako. Toka nje ukawaingize watu ndani.

34 Mungu anafanya mambo makubwa zaidi siku hizi kuliko yaliyowahi kujulikana tangu Yesu Kristo alipokuwa duniani. Hiyo ni kweli. Nalo linapita moja kwa moja juu ya vichwa vya watu, nao wanakosa kuliona. Hiyo ndiyo sehemu mbaya.

35 Laiti wangalilijua, kama vile Yesu alivyosema—alivyosema kuhusu ninii—ninii . . . kasema, "Laiti ungaliijua siku yako, laiti ungaliijua tu! Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya, kama vile kuku awakusanyavyo vifaranga wake, lakini hamkutaka. Laiti ungaliijua tu siku yako, kujiliwa kwako!"

36 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Daima imekuwa hivyo; hivyo ndivyo ilivyo sasa. Laiti tungalijua tu siku ya kujiliwa. Lakini kujiliwa kunaendelea moja kwa moja, nao watu wanaangalia mbali sana *huku* wakitafuta *kitu kingine*. Na muda si muda mwajua, kule kujiliwa kumekwisha, na ni hayo tu.

37 Lakini kama Yeye alivyosema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Amina. Loo, hilo ndilo linalotufanya . . .

38 Sasa, tunapenda kuzungumza na watu ambapo tunaweza kuwafanya wajisikie vizuri sana. Lakini jambo bora zaidi la kufanya, kama kuna—kuna kasoro, hebu na tuliondoe hilo njiani kwanza. Hebu tuingilie kitu hicho kwenye msingi. Mnaona?

39 Jamaa fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, mhudumu anayejulikana sana, mmoja wa walio bora kuliko wote ulimwenguni, akasema, "Ndugu Branham, unafanya kosa kubwa kupita kiasi."

Nikasema, "Samahani, ndugu yangu, niambie liko wapi."

40 Kasema, "Unawakemea watu kupita kiasi," kasema, "wewe, kwa mfano, wewe—wewe daima unawakemea wa—wanawake kwa jinsi wanavyovalia, nawe sikuzote unakemea *hili* na *lile*." Akasema, "Afadhali uachane na hayo. Utaharibu huduma yako."

41 Nikasema, "Wakati wowote Neno la Mungu linapoiharibu huduma yangu, Mungu, iharibu upesi sana, kwa sababu na—nataka iharibike." Hiyo—hiyo ni kweli. Ninataka kutoa kitu kilicho sahihi. Neno la Mungu linafundisha hilo.

42 Nami ninasema, "Mungu atupe ujasiri, na watu watakaoitetea ile kweli, bila kujali kijacho ama kiendacho." Hilo ndilo tunalohitaji. Injili si kitu cha dondoadume; Injili ni kwa ajili ya wanaume, wanaume walioitwa na Mungu.

43 Kamwe humtambui mwanamume kwa ukubwa wa mikono yake, na jinsi mabega yake yalivyo mapana. Ninawasikia wakisema, "Loo, hivi yeye si ni mwanamume kweli." Nimewaona watu waliokuwa na uzito wa ratili mia mbili, hawakuwa na angalau wakia moja ya mwanamume ndani yake. Hiyo ni kweli. Humpimi mtu kwa ukubwa wake. Huo ni unyama. Unampima

kwa tabia yake. Kamwe hapajakuwapo na Mtu mwenye tabia kuu kuliko Yesu Kristo.

44 Mwili mkubwa, nyumbu ni mnene kuliko mtu yeyote, kwa hiyo usingeweza, ama ndovu, kwa hiyo, wewe... huo ungekuwa ni unyama. Lakini mtu si kwamba ana misuli mikubwa kiasi gani. Simpimi kwa hiyo, bali jinsi makovu yalivyo kwenye magoti ya suruali yake, ambapo amekuwa akiomba. Huyo ndiye mtu anayepaswa kupimwa: tabia.

45 Yesu alikuwa Mtu mdogo, Jamaa mdogo, labda aliyeinama mabega. Kwenye umri wa miaka thelathini, alionekana mwenye umri wa miaka hamsini, Biblia ilisema. Lakini hapajakuwapo na mtu duniani kama Yeye, wala hatakuwako kamwe. Yeye—Yeye... Biblia ilisema, "Hakuwa na uzuri hata—hata tumtamani. Tulipomwona tuliuficha, tuseme, uso wetu Kwake," na yote namna hiyo.

46 Lakini hata hivyo, ilimpendeza Mungu ku—kumpiga. Naye alipigwa, akapigwa, na kuteswa. Yeye alichukua makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Loo, inapaswa kuwavutia watu. Kweli inapaswa. Inapaswa kuuchochea moyo.

47 Lakini mnajua shida ni nini? Tumeuondoa mkutano wa maombi ya Jumatano usiku, na kuweka kipindi cha televisheni ambacho huwatumbuiza watu wote. "Na ulipo moyo, ndipo ilipo hazina, hapo ndipo ulipo moyo pia." Basi ni kitu gani kinachowafanya watu wapende kuyaendea mambo ya ulimwengu? Vema, mimi... Mnajua, sababu ya ninyi kufanya hivyo? Ni... Sababu ya watu kufanya hivyo? Ni kitu gani kinachomfanya mtu apende kulewa? Ni kitu gani kinachowafanya watu wapende kutenda jinsi wanavyotenda? Ulimwengu. Mtu angekaaje nyumbani Jumatano usiku asiende kwenye mkutano wa maombi, kuangalia kipindi fulani cha televisheni, wangefanya hivyo kwa sababu gani?

48 Ni kwa sababu kuna kitu ndani yao kinachotamani kuridhishwa. Wanataka... Kuna mahali padogo moyoni mwa mwanamume ama moyoni mwa mwanamke, na Mungu alipafanya mahali hapo kwa ajili yake Mwenyewe. Unathubutuje kujaribu kuchukua mambo ya ulimwengu na kuyaweka humo ndani ambapo Mungu alijifanyia Mwenyewe pa kuketi humo.

49 Mungu ndiye furaha yetu. Mungu ndiye raha yetu. Mungu ndiye utoshelevu wetu. Hapo ndipo mahali pake, *hapa* ndani; mkaribishe Mungu, ndipo mambo hayo mengine yamekufa sana, hata huyajali tena.

50 Loo, watu ni wa kidini sana, daima wamekuwa hivyo. Kama nilivyohubiri hivi majuzi usiku kule, uamsho daima huzaa mapacha, kama vile Esau na Yakobo: mtu wa ulimwengu, na mtu

anayetamani haki ya mzaliwa wa kwanza. Mnaona? Daima, kila uamsho husababisha jambo hilo.

51 Uamsho huu wa siku za mwisho, umefanya jambo lile lile. Ni kweli. Kwa hiyo hebu na tuingie upande wa Yakobo, yule atakayerithi, yule anayeenda katika nchi ya ahadi. Nasi hatuwezi kuridhika tu na kwenda kanisani na kuandika jina letu kwenye kitabu. Tukiridhika, kuna kasoro. Hebu tuendelee kupanda juu zaidi na zaidi, mpaka tutakapoifikia nchi hiyo ya ahadi.

52 Huku nikihubiri hivi majuzi kwenye mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo huko Phoenix, Arizona, huko katika—katika ukumbi wa michezo, nilisema, "Waisraeli hawangeweza kamwe kuwazia, walipokuwa wakipaza sauti na kucheza katika Roho, huku Miriamu akiwa na tari hiyo baada ya kuvuka Bahari ya Chumvi, na kuwaona wale wanyapara wamekufia nyuma yao, hawakuwazia hata kidogo walikuwa mbali na nchi ya ahadi kwa miaka arobaini." Wasingeweza kuamini hilo. Walikuwa umbali wa yapata siku nne tu.

53 Lakini iliwabidi kuwa na, mwajua, iliwabidi kwenda hadi kwenye Kutoka 19 na kufanya kosa lao kubwa kuliko yote waliyopata kufanya: iliwabidi kwenda na kuchukua sheria, kusudi wapate kuzozana na kuunda madhehebu, na kujikusanya pamoja.

54 Neema ilikuwa imewapa nabii. Neema ilikuwa imewapa mwana-kondoo. Neema ilikuwa imewapa miujiza. Neema ilikuwa imewapa uamsho mkubwa sana waliowahi kuwa nao. Neema ilikuwa imewapa vitu hivi vyote, na hata hivyo walitaka sheria.

55 Hapo ndipo hasa ambapo baba zetu walisimamia katika Pentekoste yapata miaka arobaini iliyopita. Neema ilikuwa imewapa. Wote walikuwa katika moyo mmoja. Kila . . . Pentekoste ilikuwa ni Pentekoste. Lakini wasingeweza kuridhika, hilo. Iliwabidi kujiundia darasa lililoitwa Assemblies of God. La, iliwabidi kujipatia lingine: Church of God, Foursquare, Umoja, Uwili, Utatu, Unne. Nanyi mmeketi papo hapo miaka arobaini. Mungu aturehemu. Tunahitaji . . .

56 Vema, walikaa pale mpaka watu hao wote wenye nia kama hiyo wakafa. Ndipo siku moja, Yoshua akasimama, akawakumbatia wote, ndipo Mungu akasema, "Mmekuwa kwenye mlima huu muda mrefu kutosha. Sasa, hebu twendeni kaskazini, tutavuka ng'ambo, tuichukue ahadi."

57 Mungu anaweza kuwachukua Wabaptisti, ama Wamethodisti, ama chochote anachotaka. Lakini mtu fulani atavuka kule. Hiyo ni kweli. Na maadamu tungali tunapata mawazo yetu ya kitamaduni na kuketi huku ambako tunaninii . . . Loo, mtakaa tu papo hapo. Hiyo ni kweli kabisa.

58 Loo, hebu tuinuke. Hebu tutoke ndani yake. Jamani, hebu tujitikise na tutambue Mungu angali ni Mungu, ndivyo alivyo, hana budi kudumu, kama Yeye aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Yeye habadilishi akazifuata njia zetu. Tunapaswa, kubadilisha njia zetu tuziendee njia Zake. Loo, hata sikutaka kusema hilo. Ninaninii tu. . .

Ni—nitasoma baadhi ya Maandiko sasa. Vema. Yohana Mtakatifu 12:20. Nitasoma tu kifungu kimoja hapa.

> *Palikuwako na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda. . .kuabudu. . .kwenye karamu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya,. . .*wakamwomba*, wakisema,* Mabwana*, sisi tunataka kumwona Yesu.*

Sasa, fungueni Waebrania 13:8.

> *Yesu Kristo ni yeye yule jana,. . .leo, na hata milele.*

Ni wangapi wanaoamini hilo kwa uchaji kwa moyo wako wote?

Sasa, kesho usiku tutaziendea ibada za kiinjilisti. Usiku wa leo tutaninii. . .tumeutenga kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu.

59 Sasa, kuna jambo moja kuzungumza juu ya jambo lolote, halafu kuna jambo lingine kuyatekeleza yale tuliyozungumzia. Na lote ni Neno la Mungu, na kitu pekee inachohitaji ni imani ya kufanya ahadi yoyote ya Kiungu ifanye kazi. Hiyo ni kweli. Kama Mungu alifanya ahadi, basi Mungu anawajibika kwa ahadi Yake.

60 Sasa, ninawatakeni mnipe tu wakati wenu mkamilifu kwa dakika chache. Kama mtanipa kama dakika thelathini, kisha tutaitisha mstari wa maombi, ndipo dakika chache, tunaweza kwenda nyumbani.

61 Sasa, jambo la kwanza ni: Je, mnaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaamini hilo, kwa uchaji? Je, Yeye ni yeye yule kwa kanuni? yeye yule katika uweza? ngu—nguvu zile zile alizokuwa nazo wakati mmoja? huruma ile ile? Kama angalikuwa hapa, ambapo Yeye yuko leo hii, hivi angetenda sawasawa kabisa na alivyotenda alipokuwa hapa hapo awali?

62 Ama, mnafikiri baada ya miaka elfu mbili Yeye amekuwa na hekima zaidi kidogo, mwerevu zaidi kidogo, anajua jinsi ya kulifanya kanisa vinginevyo? Na kwa namna fulani ingembidi Yeye kuomba msamaha kwa yale aliyofanya kwenye—kwenye kanisa la Kipentekoste kwanza, ili kwamba ajifanyie tu kanisa tofauti la Kipentekoste la wakati wa mwisho? Hilo lingekuwa ni wazo Lake?

63 Sivyo kama Yeye ni yeye yule. Angekuwa na mawazo yale yale. Naye alikuwa ni Mungu, kwa hiyo hawezi kubadilika. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Kwa hiyo angekuwa na mawazo yale yale, na kanuni zile zile, nguvu zile zile, na Kanisa lile lile. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

64 Sasa, siku moja kulikuwa na watu ambao hawakuwa wamemwona kamwe, wakayumbayumba wakaingia mkutanoni, ama, wakaenda kuabudu kwenye Pentekoste. Walikuwa wamesikia habari Zake. Kwa hiyo wakamjia mmoja wa watumishi Wake na kusema, "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Na kwa kumwomba mtumishi huyu, mtumishi huyu aliwaletea Yesu.

65 Sasa, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, nawe umeinua mikono yako kwamba ungetaka kumwona, basi kwa nini hatuwezi kumwona? Hilo ndilo swali. Hivi hatuwezi kumwona? Kama Yeye ni yeye yule, basi kwa nini hatuwezi kumwona?

66 Wewe uliinua mkono wako kama hao Wayunani. Ungetaka kumwona. Ninainua mkono wangu. Ningependa kumwona Yeye. Naye aliahidi ya kwamba atakuwa pamoja nasi wala hatatuacha kamwe. "Niko pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari." Daima yuko hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi kuna shida gani? Kwa nini hatuwezi kumwona?

67 Sasa, kama Yeye atakuja miongoni mwetu usiku wa leo . . . Sasa, kama wewe ni mgeni huenda usielewe hili, bali ninakutaka ushushe tu masharafa, na kutulia kwa ajili ya—kwa ajili ya mkutano huu wote, na kusikiliza kwa makini Maneno haya, ahadi nitakazowasomea, zilizoandikwa hapa katika . . . kwenye karatasi hii, kutoka kwenye Biblia. Nami na—nataka kuwasomea ahadi kadhaa tuone kama Yeye angali hai au la, tuone kama dini yetu ya Kikristo ndiyo dini ya kweli, na kama dhana yetu ya Kipentekoste juu yake ni kweli, ama kama si sahihi.

68 Hata, ninaamini katika, sasa, hata katika makosa yake yote, bado ninalichagua kuwa ndilo kanisa, sasa, sio kwa sababu wao ni Wapentekoste. Pentekoste si dhehebu. Sasa, ninyi Wabaptisti na Wamethodisti kumbukeni jambo hilo, Wakatoliki na Wapresbiteri, hamwezi kumwundia Mungu dhehebu. Humwundii Mungu dhehebu. Pentekoste ni tukio ambalo Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki, na *wote* hupokea.

69 Sasa, daima nimesema, "Kama mtu ni Mkatoliki, naye anategemea kanisa Katoliki kwa ajili ya wokovu, amepotea. Na kama yeye ni Mbaptisti na analitegemea kanisa la Kibaptisti kwa ajili ya wokovu, amepotea. Kama yeye ni Mpentekoste

na analitegemea kanisa la Kipentekoste kwa ajili ya wokovu, amepotea.

70 Lakini kama yeye ni Mkatoliki na anamtegemea Yesu Kristo, anaokolewa kwa imani, imani yake mwenyewe. Kama yeye ni Mbaptisti, ama Mpentekoste, naye anamtazamia Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu, kwa kuwa ni kwa imani mnaokolewa, na hiyo ni kwa neema ya Mungu, hiyo ni kweli, imani yako binafsi katika Yesu Kristo ndiyo inayokuokoa.

71 Sasa, kama hiki ndicho Kitabu Chake. . .Nilikuwa na mahojiano si muda mrefu uliopita na kasisi wa Katoliki. Alikuja nyumbani kwangu kuuliza kama nilimbatiza msichana fulani ambaye. . .alipokuwa mtoto mchanga, ama, msichana mdogo mwenye umri wa kama miaka kumi na mitano, alikuwa ameolewa tena, na kuolewa tena na Mkatoliki. Naye. . .ilimbidi kumbatiza tena. Askofu aliniuliza maswali kadhaa. Naye akaniuliza kama nilimbatiza, nami nikamwambia, "Ubatizo wa Kikristo kwa kuzamishwa."

Naye akasema, "Kanisa Katoliki lilikuwa likifanya hivyo."

Nikasema, "Lini?"

Kwa hiyo akarudi na kusema, "Katika siku za Biblia."

Nikasema, "Basi unadai ya kwamba Bi—Biblia ni. . .Kanisa Katoliki liliandika Biblia?"

72 Kasema, "Yesu Kristo aliliundia kanisa Katoliki dhehebu na kumweka Petro kuwa kichwa chake na wale mitume kumi na wawili; na hilo lilikuwa ndilo kanisa Katoliki la kwanza."

73 Nikasema, "Basi kama haliwezi kukosea, wala halibadiliki, kwa nini kumekuwa na mabadiliko mengi zaidi yaliyofanywa? Mbona, mna wanawake elfu kumi hapa nje mnaowaomba, watu waliokufa. Na kuna Mpatanishi mmoja tu, ilisema Biblia, kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Mwanadamu, Kristo Yesu, hakuna akina Mariamu, wala chochote kile. Unaona?" Nikasema, "Kwa nini?"

Akasema, "Vema, unaona, Bw. Branham, hatupaswi kubishania Neno."

74 Nikasema, "Sibishanii Neno. Ninakuuliza tu." Nikasema, "*Nina Babeli Mbili* cha Hislop. Nina historia za kale sana ninazoweza kupata. Hawa hapa *Wazee wa Nikea*, Baraza la Nikea, Baraza Lililotangulia Nikea, na vyote, papa hapa katika chumba changu cha kusomea. Nionyeshe mahali popote palipokuwa na kanisa Katoliki mpaka mwaka wa 305. Nionyeshe lilipokuwa."

Akasema, "Unanukuu historia."

75 Nikasema, "Ninajuaje kulikuwako na George Washington hapa, kwa historia tu? Nionyeshe kitu tofauti." Mnaona? Nami nikasema, "Hiyo ni kweli kabisa. Mungu kamwe hakuliundia

kanisa dhehebu, wala kamwe haukuwa mpango wa Mungu kulifanya." Kanisa mama la madhehebu ni Katoliki, na hayo mengine yote yametoka kwenye madhehebu yale yale kulingana na Ufunuo 17. Hiyo ni kweli kabisa.

76 Kuvunja ushirika! Sisi sote ni mmoja, Pentekoste ni kwa ajili ya Methodisti, Baptisti, Katoliki, Presbiteri, "Yeyote atakaye, na aje, anywe kutoka kwenye chemchemi ya maji ya Uzima bure." Kweli. Sasa, kama Yesu ndiye. . .

77 Sasa, sizungumzi dhidi ya madhehebu haya, lakini unapoweka ua dogo kuzunguka. . .Ni kama kitu kidogo nilichoona wakati mmoja, maskini tumbili mdogo ameketi juu ya mti. Naye akasema, akawaangalia maskini tumbili hao wengine, kasema, "Unajua wanatwambia kwamba. . . wanatwambia, ama, wanasema kule chini ya kwamba—ya kwamba walitokana na sisi." Akasema asingeweza kuamini hilo.

78 Kasema, "Je, ningeuzungushia mti wangu ua hapa ili kwamba tumbil' mwenzangu asiweze kuja na kuchuma nazi wakati alipoitaka? Je, ningesema kwamba mimi ndiye tumbil' pekee aliyeko kwenye—kwenye miti?" Vema, kasema, "Kama ndivyo, basi jamii ya tumbili imeanguka." Hiyo ni, vema, hiyo karibu ni kweli pia. Naam.

79 Tunapojaribu kukiwekea kitu ua. . .Mungu hakiwekei ua. Yeye huvunja nyua, hubomoa ukuta wa kati uliotutenganisha na, wote katika mmoja katika Kristo Yesu. Roho Mtakatifu ni kwa ajili yetu sote, ili sote tuweze kuuona utukufu wa Mungu.

80 Katika mikutano yangu yote sijawahi kumwona akisema, "Vema, jamaa huyu ni Mpresbiteri, kwa hiyo hawezi kuponywa. Na huyu ni Mbaptisti, kwa hiyo hawezi kuponywa." Yeye hawaponyi watu namna hiyo. Ni juu ya msingi wa imani yao wala si madhehebu yao. Kweli.

Sasa, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele. . .Kanisa Katoliki lingesema, "Hakika, tunaamini hilo. Tunaamini hilo kanisani mwetu."

Wabaptisti wangesema, "Tunaamini hilo kanisani mwetu."

Wakatoliki waseme, "Tunaamini jambo hilo" katika kanisa hilo.

81 Sasa, kama ningeiwekea msingi hotuba hii juu ya Baptisti, kanisa ninalotoka, ama kama nilitaka kuiwekea msingi juu ya Pentekoste, ama kama nilikuwa nikitaka kuiwekea msingi juu ya mojawapo ya madhehebu ya Pentekoste, afadhali niache. Hivyo tu.

82 Lakini kuna jambo moja tu la kufanya. Hapana budi kuwe na kitu fulani sahihi na kisicho sahihi. Ni kweli kabisa. Huwezi kupata kosa na sahihi wakati uo huo. Tuna dola bandia kwa sababu ilitengenezwa kutoka kwa dola halisi.

Sasa, to—tofauti ni nini? Tungejuaje basi? Kanisa Katoliki linasema, “Sisi ndio dhehebu la kale kuliko yote.”

Pentekoste ikasema, “Mbona, tulianza kule nyuma kabla ya madhehebu.”

Vema, tutaendelea tu na *haya* yote.

Mbaptisti alisema, “Tulianza kutoka kwa Yohana. Alikuwa ndiye Mbaptisti wa kwanza, hata kabla ya Yesu kuja jukwaani.”

Vema, mngekuwa na mabishano ya kila namna. Lakini hebu tulifuatilie tuone.

83 Sasa, vipi kama tukishuka kwenda katikati ya mji kumtafuta Yesu, kwamba Yeye ni yeye yule? Tungemwona mtu akija amevaa joho kama alilovaa Yeye, na hili—na wazo hili lake la kisaikolojia kwamba Yeye alikuwa na nywele ndefu. Hatuna kumbukumbu ya hilo, kwamba Yeye alipata kuwa na nywele ndefu. Hatujui.

84 Lakini tuseme tulimwona—kweli tulimwona mtu aliyefanana na picha ya msanii aliyochora ya Yesu, naye alikuwa na makovu mikononi mwake, makovu miguuni mwake, na—na alama za miiba, na kadhalika, na ilionekana kama, labda, picha Yake ya Hofmann, ilikuwa ni *Kichwa cha Thelathini na Mitatu,* ama labda baadhi ya hizo zingine, kama zile za uvuvio, ama—ama picha fulani, huyo bado asingeweza kuwa ni Yesu, kwa sababu nitawaambia ni kwa nini: Kwa sababu hakuna mtu atakayemwona Yesu duniani katika mwili wa kawaida mpaka kwanza Yeye aingie utukufuni; kwa sababu tutanyakuliwa kumlaki hewani. Hiyo ni kweli.

Loo, Yeye alisema katika siku za mwisho, kutakuwako na Makristo wa uongo, na kila kitu kikisema, “Lo, Yeye yuko jangwani; katika chumba cha siri; msiamini.”

85 Lakini Yeye yuko hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, na Roho aliyekuwa ndani ya Kristo atafanya mambo yale yale aliyofanya, kwa sababu ni Uzima ule ule. Ukiweka uhai wa—wa mzabibu katika mtango, utazaa zabibu. Kama ukiweka uhai wa mpichi katika m—mkuyu, utazaa mapichi. Unaona? Kweli kabisa. Kwa sababu huo ndio uhai uliomo ndani yake, unaozaa.

Nao Uhai ulio katika Kanisa la Yesu Kristo utazaa kazi na alama za Yesu Kristo.

Nalo Kanisa ni mtu binafsi. Mungu hushughulika na Israeli kama taifa, bali Mataifa kama watu binafsi. Sasa, mnalipata, sivyo? Mnaona? Mtu binafsi . . .

Taifa—taifa litaokolewa wakati Israeli itakapokuja. Litazaliwa tu katika siku moja wakati Israeli itakapomjia Mungu wakati mmoja.

Lakini basi, wakati Mataifa, ni mtu binafsi. Watu aliowatoa kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake, akimfanya Bibi-arusi Wake.

86 Sasa, tungefanya nini basi usiku wa leo kama tulitaka kujua Yeye yuko katika kanisa la nani? Kama nilitaka kuona kama Yeye yuko katika kanisa la Kipentekoste, kama nilitaka kuona Yeye yuko katika kanisa la Kibaptisti, ama kanisa Katoliki (dhehebu la kale kuliko yote), ama ni lipi ninge. . .? Lutheri, hilo linafuata Katoliki, na Wesley linafuata, na kuendelea mbele namna hiyo. Kama ningeenda kule, niyaangalie hayo makanisa, ningetarajia nini? Mtu ambaye angefanana na Yeye? La. Huenda kukawa na watu wengi wanaofanana Naye, kabisa. Ningetarajia nini?

87 Basi ningemtafuta mtu aliyekuwa na Uhai ndani yake. Ningetafuta Kanisa lililokuwa na Roho ndani yao kama tu Roho Wake. Mnaona? Ningeangalia nione kazi Zake. Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi (Yohana Mtakatifu 14:12), Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hiyo ni kweli? Basi sisi . . . Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

88 Sasa, mnaona katika tafsiri pale, ilisema, "Kubwa kuliko hizi atafanya, ataninii. . . " lakini, kwa kweli, tafsiri sahihi kutoka kwake ni. . . Ninayo *Kamusi Asili*, nayo inasema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya, na *nyingi* kuliko hizi atazifanya," sio kubwa zaidi, maana wasingeweza kufanya kubwa zaidi. Aliwafufua wafu, akawaponya wagonjwa, akakomesha maumbile. Hakuna kitu kingeweza kuwa kikubwa zaidi. Lakini si—si katika ubora, bali katika *wingi* Yeye angeweza kuwa mkubwa zaidi.

89 Kwa sababu wakati huo Yeye. . . Mungu alikuwa ndani ya Mtu mmoja, Kristo Yesu; katika Yeye ulikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Sasa, wakati ile Nguzo ya Moto iliposhuka kwenye Pentekoste, mnaona, Ndimi za Moto zilikaa juu ya kila mmoja wao. Kabla hawajaanza kunena kwa lugha, kulikuwako na Ndimi za Moto. Huyo alikuwa ni Mungu akijitenga Mwenyewe kutoka kwa Nguzo ya Moto kuingia ndani ya kila mshiriki wa Kanisa Lake. Mungu akijitenga Mwenyewe kusudi aweze kuwa ulimwenguni kote kila mahali kwa wakati mmoja.

90 Hivi sasa mikutano ya uponyaji inaendelea Afrika. Viwete wanatembea, vipofu wanaona, kote ulimwenguni, Kanisa la ulimwenguni kote la Bwana Yesu Kristo katika watu binafsi, watu wanaoishi na kumtumikia Yeye. Mungu alijitenga na kujiweka Mwenyewe miongoni.

91 "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, na Baba ndani Yangu, Mimi ndani yenu nanyi ndani Yangu." Mnaona? Mnaona? "Nitakuwa. . . Bado kitambo kidogo na ulimwengu (kosmos kule, utaratibu wa ulimwengu), hautaniona tena. Hata hivyo ninyi, Kanisa, mtaniona, kwa kuwa Mimi, *Mimi* ni 'kiwakilishi nafsi,' nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu,

hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli. "Mimi, nitakuwa pamoja nanyi. . . " Mnaona, Kanisa la ulimwenguni kote la Bwana Yesu Kristo. "Nitakuwa pamoja nanyi. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya."

92 Sasa, hebu na tuwazie kwa dakika moja tu yale aliyofanya wakati huo. Hebu tuone ni kazi za aina gani alizofanya, na jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe. Sasa, tunachukua, kwa mfano, Yeye aliitwa Masihi. Na *Masihi* maana yake ni, "Aliyetiwa Mafuta," Kristo. Alikuwa ameahidiwa tangu bustani ya Edeni, huko nyuma katika Mwanzo.

93 Sasa, tunarudi tu nyuma tuone. Sasa tu—tunasoma usiku wa leo kutoka katika Yohana Mtakatifu 12. Hebu na turudi kwenye Yohana Mtakatifu 1, na ndipo tutaona Yeye alikuwa ni nani. Na kama tunaweza kuona kile alichokuwa, na alikuwa wa kanisa gani, alihudhuria dhehebu gani, basi kama ni shirika letu tunaweza kuridhika nalo.

94 Nasi tutaona kile alichokuwa, na kile alichokuwa wakati huo, na kile alichofanya wakati huo, anapaswa kuwa kitu kile kile, na kufanya jambo lile lile leo, kwa sababu Yeye alisema angefanya. Je, hilo lingeliridhisha kanisa? Vema sasa, hebu turudi tu nyuma tuone.

95 Sasa, nitanukuu, nanyi mkasome. Wakati—wakati mtakapoenda nyumbani, chukueni milango hii ninavyoirejea hapa. Halafu basi, tunapokuwa na. . . tulitaka kuwa na ibada ya siku zote ya uponyaji, tuendelee tu kuchambua kutoka Mwanzo hadi Ufunuo kuonyesha ya kwamba hii ni kweli.

96 Sasa, huenda ukawa na mawazo yako yasiyobadilika kabisa (vivyo hivyo na Mafarisayo) juu ya yale Masihi angefanya wakati atakapokuja. Lakini Yeye alikuja tofauti kidogo. Hata hivyo Yeye alikuja jinsi Maandiko yalivyosema hasa, jinsi Yeye. . . wao. . . Maandiko yalisema angekuja. Sasa, hebu na tumwone kwa dakika moja.

97 Tunaona, baada ya kuzaliwa Kwake, hadi kwenye umri wa miaka thelathini, binamu Yake wa pili, Yohana, alikuwa akibatizia nyikani. Ndipo Yesu akashuka chini na akabatizwa, nazo mbingu zikafunguka, naye akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua. Naye akaenda nyikani akajaribiwa na. . . siku arobaini na ibilisi, akarudi na huduma Yake.

98 Ndipo jambo la kwanza aliloanza kufanya, tunaona hapa katika Yohana 1, alianza kwenda huku na huku akiwaponya wagonjwa. Ndipo kulikuwa na mtu jina lake Andrea aliyekuwa amemwamini. Hebu tumchukue kwa muda kidogo tu. Hebu na tuchukue sasa jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi.

99 Sasa, kumbukeni ya kwamba Mungu daima hutoa ishara na maajabu. Ni wangapi wanaoamini hilo? Sasa, katika Agano la Kale. . . Sasa, sikilizeni kwa makini. Kab-. . . Haitachukua muda mrefu. Kama tunaweza kuwafanya muuone Ujumbe,

ninyi. . .hakutakuwa na mtu hapa ndani kwenye kiti cha magurudumu. Hakutakuwako na mgonjwa katika jengo hili katika dakika arobaini tangu sasa, kama mtasikiliza na kulishika kwa makini.

Sasa, hebu na tulithibitishe. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. "Thibitisha mambo yote." Sasa, kama Yeye alifanya ahadi, hana budi kuitimiza hiyo ahadi.

100 Naye Mungu, katika Agano la Kale, kama nabii alitabiri, ama mwotaji aliota ndoto, jinsi walivyojua kama hiyo ilikuwa ni kweli ama si kweli, walishuka wakaenda kwenye Urimu Thumimu. Wachungaji na kadhalika wanajua jambo hilo, kile kifuko cha kifuani cha Haruni. Alikuwa na yale mawe kumi na mawili ya mawe ya kuzaliwa ya wale wazee wetu. Kilitundikwa kwenye nguzo hekaluni. Ndipo wakati nabii alipoanza kutabiri, ama mwotaji kusimulia ndoto, haidhuru ilisikika halisi jinsi gani, kama hakikuonyesha msongamano huo wa nuru mle ndani, ya kimbinguni hayakuwa yakitenda kazi, kwa hiyo waliukataa huo ujumbe.

101 Sijali unasikika mzuri jinsi gani, jinsi unavyolingana na theolojia ya Dk. *Fulani-wa-fulani*, ama jinsi ulivyoafikiana na. . .kanisa *hili* ama dhehebu *lile*, waliuhukumu kwa sababu ya kimbinguni hayakutenda kazi. Amina.

102 Ninaanza kujisikia kubarikiwa. Naam, bwana. Alipo Mungu wa Kimbinguni, kutakuwa na mambo ya kimbinguni yakitendeka. Kamwe huwezi kujiepusha nayo. Haina budi kuwa hivyo.

103 Sasa, angalia, sasa, wakati huo ukuhani ulipokwisha, ukuhani wa Haruni, ndipo hiyo Urimu Thumimu iliondolewa. Lakini Mungu ana Urimu Thumimu nyingine, ambayo ni Neno Lake, Biblia.

104 Sasa, kama Mungu anatoa ahadi katika Biblia, halafu basi kama ukiipokea hiyo, ahadi ya kimbinguni itafanya dhihirisho la kimbinguni, maana Mungu atalithibitisha Neno Lake. Kweli kabisa. Kama sivyo, basi si Neno la Mungu. Ikiwa sivyo. . .

105 Basi—basi kama imani yetu si kubwa vya kutosha, usiikane, kama Mungu alitoa ahadi, aseme, "Ni kweli, bali sina imani ya kutosha kufanya hivyo," hebu jamaa huyo mwingine alifanye.

106 Kama sina imani ya kutosha kuanza kutembea kama Henoko alivyofanya, kufanya matembezi ya alasiri na kwenda Nyumbani pamoja na Mungu, kamwe sitasimama katika njia ya mtu mwingine ambaye ana imani ya kutosha kufanya hivyo. Nitasema, "Mungu asifiwe kwa ajili ya ndugu huyo, alitembea moja kwa moja akatoka duniani, ninashukuru tu kwa hilo, si—siwezi kufanya hivyo, lakini yeye. . .Ninashukuru alifanya hivyo. Mimi. . . " Mnaona? Ninaamini hilo, wala sitaki kumzuia mtu yeyote aliye na imani ya kulifanya Neno la Mungu lithibitishwe. Sasa, halina budi kutoka kwenye Neno.

107 Sasa, Yesu alipokuja, alikuja kwa walio Wake, Wayahudi. Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alikuwa na ishara ya Masihi iliyomfuata. Yohana alishuhudia jambo hilo, naye alionekana kama hu—hua, Nuru, ikishuka kutoka Mbinguni. Aliona jambo hilo. Sasa, wakati Nuru hiyo, ama hua, alipoingia ndani ya Mwana wa Adamu, tunaona kilichotukia.

108 Andrea, hebu tuanze naye. Sisi. . .Sasa, katika Yohana Mtakatifu 1, mlango wa kwanza, niko ndani. Tunaona ya kwamba Andrea, mara alipomwamini Bwana Yesu Kristo, anaenda kumchukua Simoni Petro. Jina lake lilikuwa Simoni wakati huo, naye akamwambia Simoni, "Sasa, huna budi kuja uone." Hebu tuingie kwenye mazungumzo yao. Wote wawili ni wavuvi.

109 Ninaweza kumwona Simoni, labda ndiye mkubwa kati yao wawili, ameketi chini kando ya mtumbwi na kusema, "Andrea, sasa unajua ya kwamba sote wawili ni Mafarisayo, kwa sababu tunamfuata baba yetu mzee, yule Farisayo. Nami ninakumbuka, Andrea, kabla baba hajakufa nilipokuwa mvulana mdogo, siku moja baada ya kuvua samaki ziwani siku nzima, tuliingia; naye baba alikuwa ameomba sana kwamba angepata samaki. Ndipo papo hapo kwenye saa ya mwisho tukavua samaki kwa ajili ya chakula chetu kesho yake. Loo, ninaweza kuona jinsi—jinsi mama daima amepiga magoti akiomba. Jinsi tulivyomtumainia Mungu kutusaidia."

"Loo, bila shaka, Ndugu Simoni. Ninakumbuka hilo vizuri sana."

110 "Vema, ninakumbuka," Simoni, "baba yangu aliniambia siku moja alipokuwa akizipapasa nywele zangu nyuma, nami nikaweka mikono yangu juu ya nywele zake zenye mvi, naye akasema, 'Simoni, mwanangu, sikuzote nimetamani kuishi kuona siku ambayo Mkombozi wetu, Masihi, angekuja. Lakini ninazeeka sasa, kwa hiyo nadhani sitaweza kumwona, Simoni. Lakini wewe ni mvulana mdogo, hapana shaka utamwona katika siku yako.

111 "'Sasa, kutakuwako na machafuko mengi, daima yako, Simoni. Kabla tu mambo ya kimbinguni kutukia, kutakuwako na mambo mengi ya uongo yatakayotokea. Lakini ninawatakeni mkumbuke jambo hili, Simoni, ya kwamba Masihi ajapo, Masihi atakuwa na ishara ya Masihi, nanyi mtamjua kwa ishara hiyo.

112 "'Musa alisema hivyo, kwa kuwa Musa alisema, ninii. . . katika, katika mlango wa—wa Kumbukumbu la Torati, tunapata jambo hili, ya kwamba Yeye alisema ya kwamba "Bwana. . ."'" Kumbukumbu la Torati 18:15, kama mkitaka kuliandika mpate kulisoma. Soma yaliyosalia ya mlango huo, ukiendelea. "'Ya kwamba "Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Itakuwa ya kwamba mtu ambaye hatamsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu."'" Mnaona?

113 "Sasa, yeye alisema, 'Sasa, kumbuka, Simoni, huenda kukawa na wasemaji hodari sana watakaoinuka. Huenda kukawa na watu mashuhuri watakaoinuka. Lakini kumbuka, kama Wayahudi, tunajua ya kwamba Mungu anatutumia Nabii, Masihi-Nabii. Na sababu. . . Sasa, tumekuwa na miaka mia nne sasa, tangu Malaki, hatujawa na manabii wowote, lakini ajapo Masihi, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii. Tutamjua kwa hilo. Sasa, usisahau hilo, Simoni.'"

114 Sasa, anasema, "Andrea, huenda ukasema huyu ni mtu mashuhuri. Anaweza kuwastaajabisha watu sana. Lakini kwangu mimi, Yeye hana budi kuwa Nabii kwa sababu Masihi. . .

"Nami nilikusikia ukizungumza juu ya mtu yule kule nyikani, na kadhalika, Yohana, yeye, labda, alikuwa ni nabii, pia, sijui.

115 "Lakini Masihi huyu atakuwa ni Mungu-Nabii. Atakuwa Nabii *na zaidi*. Yeye atakuwa zaidi ya nabii, atakuwa Nabii *na zaidi*. Nitaambatana nawe siku moja."

116 Ninaweza kuwazia nikimwona Andrea, basi, akienda kwenye ibada kumsikiliza Yesu wa Nazareti, kisha anakuja nyumbani na kumwambia mambo fulani yaliyotukia. Kwa hiyo kesho yake labda Simoni aliamua angeenda.

117 Nanyi mnakumbuka, alipewa funguo, Simoni alipewa, baadaye. Alikuwa ni mtu asiye na elimu. Hakutoka kwenye yoyote ya seminari hizo, yoyote ya shule zao za Biblia. Hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, Simoni Petro. Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa, bali walitambua ya kwamba alikuwa pamoja na Yesu. Sasa, hilo ndilo jambo muhimu. Hiyo ndiyo Pentekoste ya kweli. Mnaona?

118 Sasa, tunaona ya kwamba alishuka na labda akatembea pamoja na Andrea, na umati mkubwa wa watu pande zote. Na mara tu alipomwona Bwana Yesu, akishangaa kama Yeye alikuwa ndiye Masihi. Sasa, tutaona Masihi alikuwa ni nani.

119 Na mara tu alipoenda Mbele ya Masihi, Yeye alimwangalia, Naye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Loo, jamani. Hilo lilimtosha. Si kwamba tu alijua yeye alikuwa ni nani, alimjua yule baba mzee mtauwa aliyekuwa amemwambia kile Yeye angekuwa. Hilo lilitosha milele. Huyo alikuwa ndiye Masihi. Naam, bwana.

120 Kama huyo alikuwa ni Masihi jana akijitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake, huyo ni Masihi leo akijitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake. Kumbukeni: kwa walio Wake. Tutalifikia hilo katika dakika moja.

121 Sasa, ilikuwa ni nini? Kulikuwa na wengi waliosimama pale, labda, hawakuelewa hilo. Lakini Simoni alijua hilo, kwa kuwa alikuwa akimtazamia Mtu wa namna hiyo. Aliongozwa na Roho.

Alijua kwa Maandiko ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi hasa. Hakumjua tu, bali alimjua baba yake, na kuyataja majina yao yote mawili.

122 Na hapo alisimama mtu mmoja jina lake Filipo, naye Filipo akasema, "Aisee, ndivyo hivyo. Ninajua huyo ni Masihi." Naye huyo akazunguka kilima, maili kumi na tano kukizunguka kilima, kumtafuta rafiki akamwambie habari zake.

123 Kuna *kitu kingine*, unapopata ono la Kristo kweli, huwezi kutulia. Huna budi kumwambia mtu fulani kulihusu. Mguso Wake tu, na unaiwasha moto nafsi yako.

"Sina budi kupata . . . Nina rafiki jina lake Nathanaeli. Yeye ni mtu mashuhuri. Yeye ni msomi mashuhuri." Naye huyo akazunguka mlima.

124 Labda ilikuwa inakaribia wakati wa jioni alipoingia. Anabisha mlangoni, ndipo Bibi Nathanaeli akaja mlangoni. "Vema, kama si rafiki yetu Filipo."

"Loo, Nathanaeli yuko wapi?"

"Anafanya matembezi huko nje katika bustani ya matunda."

125 Huyo akaenda kwenye hiyo bustani, naye akaona, huko nje chini ya mtini, akamkuta Nathanaeli amepiga magoti, labda, akisema, "Ee Bwana Mungu, ulituahidi ukombozi. Tunautazamia. Tumekuwa tukiungojea. Utafanya jambo hilo lini, Ee Bwana Mungu? Ninaingojea ahadi hiyo uliyotoa." Anaamka, na kukung'uta nguo za—zake namna *hiyo*, kisha akageuka, na ni nani aliyekuwa amesimama pale ila Filipo.

Akasema, hapana shaka, "Filipo, rafiki yangu."

126 Na kabla hajasema lolote, "Unaendeleaje? Je, miti iko sawa?" alikuwa na ujumbe wa dharura, kitu halisi. Akasema, "Njoo, umwone Yule tuliyempata." Loo, moja kwa moja kwenye alama. "Njoo umwone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu. Yeye ni Masihi. Ninajua Yeye ndiye Masihi."

127 Loo, sasa, ninaweza kumwazia Nathanaeli akisema, "Sasa, Filipo. Sasa, ninajua yale masomo mengi ya Biblia ambayo tumekuwa nayo, masomo mengi mazuri ambayo tumekuwa nayo pamoja. Nasi tunajua, mimi na wewe tunajua . . .

128 "Sasa, imekuwaje, Filipo? Je, umeingia wazimu mahali fulani? Vema, umepatwa na nini, Filipo? Sasa, usije ukaniambia ya kwamba—ya kwamba Masihi huyu angeweza kamwe kutoka Nazareti. Sasa, tunajua, tulisikia hotuba ya mwisho ya Kayafa, ya kwamba siku moja Masihi angekuja, na labda angetua na kitu kama ndege, mwajua, moja kwa moja kwenye turubai za hekaluni.

129 "Angekuja kwenye dhehebu letu, maana ndilo kubwa kuliko yote nchini. Naye angekuja moja kwa moja . . . Na iwapo hatakuja kwetu, hatutaamini. Hatutakuwa na uhusiano wowote

nalo, hatutashirikiana na hao wengine. La. Inabidi. . . Yeye atakuja kwetu. Sisi ndio. Naye atakuja huko nje, na atamjia Kayafa, kuhani mkuu, askofu wetu, na kusema, 'Mimi ndimi Masihi. Nimekuja sasa kuchukua mamlaka.' Hakika hivyo ndivyo itakavyotukia."

130 Wazo hilo halijawahi kuwaacha watu. Hiyo ni kweli. Lakini unajua nini? Mungu hufanya mambo jinsi anavyotaka kuyafanya. Kwa kawaida yeye hufanya kinyume na jinsi sisi sote tumejiandaa kulipokea, kwa hiyo Yeye angeweza—Yeye angeweza . . .

131 Vema, Yeye—Yeye amejificha Mwenyewe kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kujifunua Mwenyewe kwa watoto wachanga ambao wangejinyenyekeza na kujifunza Kwake. Sasa, upesi, angalia kilichotukia.

Lakini ninaweza kumsikia Filipo akimwendea na kitu fulani ambacho kilikuwa hakika, si maneno fulani aliyokuwa amesema, bali jambo alilokuwa amefanya.

Sasa, ninamsikia akisema, "Nathanaeli, wewe ni msomi wa Maandiko."

"Naam, bwana."

"Masihi atakuwa Mtu wa aina gani?"

"Mbona, Masihi atakuwa ni Nabii."

132 "Naam, bwana, hiyo ni kweli, kwa sababu Musa alitwambia, kiongozi wetu, yeye alikuwa, ama, maneno yake tumeyategemea, na tunapaswa kuyategemea, mpaka akaja Nabii. Naye angekuwa ndiye Masihi, na angeonyesha ishara ya Masihi."

"Naam."

133 "Vema, huyu Yesu wa Nazareti ninayenena habari zake . . . Mnamkumbuka yule mzee mvuvi huko chini wanayemwita Simoni, uliyenunua samaki kutoka kwake wakati ule, naye hata asingeweza kutia sahihi risiti yake?"

"Loo, naam. Nilimjua, pia nilimjua baba yake vizuri."

134 "Vema, hivi majuzi ndugu yake alimleta kwenye kusanyiko ambapo Yesu alikuwa amesimama. Akaangalia kote, akasema, 'Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona.' Unawajua wote wawili."

"Na Yeye alifanya hivyo?"

"Naam."

"Ni nani aliyemwambia habari zake?"

135 "Hakuna. Simoni aliletwa tu na Andrea, ndugu yake, akaja kule. Unajua halingenishangaza ila kwamba Yeye angekwambia wewe ni nani utakapofika kule."

"Vema, sijui kuhusu hilo sasa. Sina budi kuona. Mwajua, nimekuwa mwothodoksi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ita—itabidi nione jambo hili."

136 Na muda si muda wajua, kesho yake walipokuja, vema, huenda walikuja kwenye mstari wa maombi, ama huenda walikuja kwenye kusanyiko. Sijui. Hata hivyo, mara Yesu alipomwona mara ya kwanza, Yesu alimwangalia moja kwa moja, akasema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake." Hilo liliondoa ugumu ndani yake. Kwamba . . .

137 Akasema . . . Sasa, labda baadhi yao walisimama karibu, kasema . . . Vema, leo wangesema, "Mbona, hakika, angejua alikuwa hivyo, kwa sababu ya vile alivyokuwa amevalia, alikuwa ni Mwisraeli." La, la. Watu wote wa mashariki walivalia sawa. Angeweza kuwa ni Mwarabu. Angeweza kuwa Myunani. Hakika, wote walikuwa weusi, walivaa mi- . . . walikuwa na ndevu na vilemba, na mavazi vile vile.

Yeye—Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake."

Loo, likamvutia sana. Akasema, "Rabi, ulipata kuniona lini Wewe?"

Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

Msikilizeni. "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Mnaona, akijitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake.

138 Sasa, kulikuwa na wale waliosimama karibu waliojiita Wake. Mmoja wao alisimama karibu Naye, naye akasema, "Unajua nini? Sina budi kutoa jibu kwa ajili ya makanisa yetu. Hakuja kwenye dhehebu letu. Kwa hiyo tutaliambia nini kanisa juu yake, wakati wao . . .? Hatuna—hatuna budi kusema jambo fulani, maana jambo fulani linatendwa. Kwa hiyo sisi . . . Tutaliambia nini kanisa letu?"

Mmoja wao akasema, "Nitakwambia." Lile baraza dogo la wahudumu kule pembeni lilisema, "Ni la ibilisi. Hiyo ni kweli kabisa."

139 Lakini wasingeweza kumficha. Akageuka, akiyatambua mawazo yao. Akasema, "Mkisema hivyo dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe hilo," lakini sasa, kulifafanua Neno hili, "lakini siku moja, Roho Mtakatifu atakuja, afanye jambo lile lile. Neno moja dhidi yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Dhambi isiyosameheka, kumwita Roho wa Mungu anayefanya kazi za Masihi, kama alivyokuwa akifanya, pepo mchafu kama mpiga ramli.

140 Kasema, "Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli. Anasoma mawazo yao. Yeye ana—Yeye ana telepathia, telepathia ya

kiakili, Naye anaweza kusoma mawazo yao. Hivyo ndivyo anavyofanya." Wasingeweza kusema Yeye hakuwa akifanya jambo hilo, maana lilikuwa pale pale, mbele za watu.

141 Lakini waangalie watu hawa waliokusudiwa Uzima. Ee Mungu! Jina lao halipatikani na mauti leo. Wako Utukufuni pamoja na Kristo. Walitambua kuwa ni Masihi. Akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Mfalme wa Israeli."

Akasema, "Kwa sababu nilikwambia hivyo, unaamini? Basi njoo uende pamoja Nami. Utaona makubwa kuliko haya." Lakini kwa sababu aliamini!

142 Sasa, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni Masihi yeye yule leo, itabidi liwe ni jambo lile lile leo kama lilivyokuwa jana. Hivyo ndivyo anavyojitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa Lake.

143 Sasa, kuna jamii tatu tu za watu duniani. Hao ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; na siku hiyo, ambao walihesabiwa kuwa Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Sasa, Wamataifa, sisi Waanglo-Sakson, tulikuwa makafiri katika siku hizo. Tuliabudu sanamu, Warumi, na kadhalika, tukiwa na marungu migongoni mwetu; wala hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Basi kumbukeni, Masihi huja tu na kujidhihirisha Mwenyewe kwa wale wanaomtazamia.

144 Sababu ya sisi kutoyaona mambo haya leo, hatuyatafuti. Tunayaangalia makanisa yetu, madhehebu yetu, taratibu zetu kuu, jinsi tunavyopanuka. Ondoa macho yako kwenye hilo. Mtazame Masihi. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

Sasa, angalia kilichotukia. Ndipo tunaona ya kwamba Yeye alikuja. Sasa, kuna. . . Yeye alifanya. . . hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi.

145 Sasa, tutachukua, tufungue kurasa kadhaa katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 4. Alikuwa akienda Yeriko. Kama mtu yeyote amewahi kuwa Palestina, ni chini ya Yerusalemu. Huko ndiko alikokuwa akienda Zake. Lakini alikuwa na haja, kupitia Samaria huko juu ya mlima. Unashangaa ni kwa nini? Sasa, katika Yohana Mtakatifu 5:19, 5:19, utasoma hili: "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda . . . " Mnaona, Yeye alikuwa ni Nabii, sehemu Yake ya Nabii. Sasa, Yeye ni zaidi ya nabii. Msifikiri ninamchukua ni nabii. Sivyo.

146 Nilimsikia Dada Florence akiimba muda mfupi uliopita. Ningependa yeye, usiku fulani, hapa chini, aimbe, *Alishuka Chini Kutoka Utukufuni Mwake*. Naupenda wimbo huo. Unaonyesha Uungu mkuu wa Yesu Kristo. Katika siku wanazojaribu kumfanya nabii tu, Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii. Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa; bali ishara Yake ya Masihi ilikuwa ni nabii.

147 Sasa, tunaona ya kwamba tunapomwona Yeye pale, amesimama pale; kisha anapanda kwenda Samaria. Sasa, Wasamaria pia walikuwa nusu Myahudi na Mmataifa, waliomwabudu Mungu. Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alienda kule juu, na ilikuwa yapata saa tano au saa sita. Aliwatuma wanafunzi Wake kununua vyakula, chakula; akashuka akaenda Samaria. Aliketi chini kisimani, labda mandhari, kitu kama picha hii nzuri hapa nyuma, ameketi pale kisimani. Kama uliwahi kuwa Samaria, na uuangalie huo mji wa umma vizuri kule, ungali upo.

148 Basi ilikuwa yapata saa tano mchana. Kulikuwa na mwanamke aliyekuja kuteka maji. Hebu tuwazie alikuwa mrembo, kama baadhi ya wanawake wa siku hizi, ila tu ilikuwa tofauti kidogo. Halafu tunaona ya kwamba yeye alininii... [Kusanyiko linacheka—Mh.] Naam. Nilikuwa nikiwazia juu yake, atakuwa na... kumfanya awe na nywele ndefu.

149 Nilikuwa nikiwazia juu ya mwanamke yule aliyeiosha miguu ya Yesu, mwajua, kwa machozi yake na kuyapangusa kwa nywele zake. Angekuwa na wakati mgumu... Ingembidi kusimama kwa kichwa chake siku hizi apate nywele za kutosha huko chini kuipangusa miguu Yake. Wamezikata zote. Biblia ilisema, "Ni utukufu wake," kwa hiyo likakatilia mbali utukufu wake. Sijui ni kwa nini. Labda alimwangalia mtu fulani hapa juu aliyemwazia zaidi, huko Hollywood. Lakini hata hivyo...

150 M—mtaniita shupavu wa dini. Mtaniita mwendawazimu mkitaka, lakini kwenye Siku ya Hukumu mtaona ni BWANA ASEMA HIVI. Sawa. Si ajabu tuna kanisa linalokufa; si linalokufa, bali lililokufa. Hiyo ni kweli. Roho wa Mungu amehuzunishwa na kuliondokea. Njia zetu zimemhuzunisha akaondoka. Tofauti zetu, na kutokumjali Yeye, ndiko kulikosababisha jambo hilo. Sitaki kuwaudhi. Siko hapa kuwaudhi. Nipo hapa kuwaamsha. Mungu aturehemu.

151 Tupe nguvu na ujasiri wa kudumu kwenye Neno la Mungu, tulilete haidhuru linamaanisha nini, linasema nini. Tunawachukua wahudumu kuleta pesa, kupatana, kuendesha vipindi vikubwa vya televisheni, na mambo kama hayo, kupatana na watu. Si mimi. Afadhali nilale kwa tumbo langu, na kunywa maji ya kijito na kula biskuti za chumvi, na kuhubiri kweli, kuliko kulazimika kusimama pale mbele ya kanisa kwenye Siku ya Hukumu, na kuhukumiwa pamoja nao.

152 Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Hazina zangu haziko katika ulimwengu huu. Hazina zangu ziko Mbinguni, na haja yangu ni watu wa Mungu, Kanisa Lake.

Usijifananishe na mke wa mchungaji fulani, ama mke wa mhudumu fulani, ama mke wa mwinjilisti. Jifananishe na Biblia. Hiyo ni kweli.

153 Siku hizi inatubidi kufanana. Mwanamke anaweza kuvaa nguo fulani kanisani, ama kutengeneza nywele mtindo fulani, na kila mwanamke anataka kuvaa kitu kile kile. Wanafanya vivyo hivyo miongoni mwa jinsia zote mbili. Sijali kama koti langu linafanana na suruali yangu au tai yangu inafanana na shati langu. Ninataka ujuzi wangu ulingane na Biblia ya Mungu. Huo ndio ulinganifu tunaohitaji siku hizi, uamsho ambao kwa namna fulani unalingana, na Roho wa Yesu Kristo akiishi miongoni mwetu.

Hiyo ni . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

154 Hawawezi kuchanganyika kama wanavyofanya hapa Los Angeles, na mahali hapa. Hawawezi kuchanganyika. Huwezi kutofautisha mmoja na mwingine sasa. Wote wanafanana. Siku hizo ilikuwa ni tofauti. Kama mwanamke alikuwa mwovu, alitiwa alama kuwa mbaya. Alikaa katika kundi lake mwenyewe; hakushirikiana na hao wengine. Sasa, ni kama tu kuchukua ya—yai na kwenda kuligonga katikati. Inafanya tu kitu hicho chote kuwa manjano. Unaona? Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo sasa.

155 Angalieni, nilikuwa nikisoma hapa ambapo metha- . . . , wapotovu, hasa, kote nchini na katika Los Angeles, jinsi ilivyo; loo, ni mbaya sana. Ongezeko lenu ni kama asilimia thelathini kuliko mwaka uliopita. Ni ninii . . . Mbona, ni Sodoma.

156 Loo, Mungu na awatikise watu hapa, hisi, uamsho mahali fulani ambao utalitikisa kanisa la Kipentekoste lijirudie tena, akitema Moto juu ya kusanyiko kusudi watu wapate kuelewa saa hii tunayoishi, limeketi limelala, kama, bila shaka Biblia ilisema wangefanya hivyo, nadhani. Vema, haya basi.

157 Sasa, mwanamke huyu anajitokeza. Naye, labda alitokea wakati huo; labda alikuwa nje usiku kucha kisha akalala mpaka wakati huo. Lakini hata hivyo, alitoka na mtungi. Akaziweka chini kamba ndogo, pamoja na kulabu ndogo, kisha akashusha winchi apate kuchota maji. Naye alipokaribia kuchota maji yake, akamsikia Mtu fulani akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

Sasa, kumbukeni yeye ni Msamaria. Sasa, Yeye aliwaonyesha Wayahudi ishara hii ya Masihi. Sasa, hawa hapa Wasamaria. "Mwanamke, nipe maji ninywe."

158 Akasema, akaangalia, naye akasema, "Mbona, sasa," nitalifanya, nitalielezea, "tuna ubaguzi hapa. Si kawaida Kwako, ukiwa ni Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho." Naye akasema . . .

159 Labda alikuwa ameketi pale, kwamba Yeye—Yeye hakuwa ila na umri wa miaka thelathini na kitu, lakini Maandiko yalisema, Yohana Mtakatifu 6, ilisema Yeye alionekana ana hamsini. Kasema, "Wewe hujapata bado miaka hamsini nawe unasema umemwona Ibrahimu."

160 Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Hiyo ni kweli. Mnaona? Labda kazi Yake ilimvunja, huenda alikuwa ameingia mvi kidogo, ama chochote kile.

161 Wakati alipokuwa ameketi pale naye mwanamke alikuwa akimwangalia, Mtu anayeonekana mwenye umri wa kama miaka hamsini ameketi kando ya ukuta huo, kasema, “Si kawaida kwenu Wayahudi kutuomba sisi Wasamaria.”

162 Akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Alikuwa akifanya nini? Sasa, itawabidi kuchukua neno langu kwa ajili ya jambo hili. Alikuwa akijaribu kuwasiliana na roho yake. Mungu alikuwa amemtuma huko chini. Mungu alinituma kwenye kanisa hili. Siwajui. Mnaona? Simjui hata mmoja wenu.

163 Lakini Mungu alikuwa amemtuma huko juu. Alihitaji kupitia Samaria. Kwa nini? Walikuwa wakimtazamia Masihi. Ilimbidi, kwenda kule na kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Kwa hiyo akaketi pale. Mwanamke huyu akasema, akazungumza Naye, kasema, kwa ajili ya hotuba, kasema, “Kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kuchotea.” Kasema, “Baba zetu waliabudu katika mlima huu, na kadhalika, na Wewe unasema huko Yerusalemu . . . ” Basi mazungumzo yakaendelea.

164 Yeye alijaribu, kufanya nini? Kuona mahali shida yake ilipokuwa. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa. Kuona shida yake ilipokuwa. Sasa, ni kitu gani? Masihi atajitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake huko Samaria (Mnaona?), kwa Wasamaria. Jinsi alivyowafanyia Wayahudi, hana budi kufanya jambo lile lile kwa Wasamaria. Hakika. Hana budi kuwaita walio Wake kwa ninii ile ile . . .

165 Mnakumbuka yale niliyosema jana usiku? Kama Mungu akiwahi kufanya uamuzi wa kufanya jambo fulani kwa njia fulani, hana budi kulifanya vivyo hivyo kila wakati. Kama hakufanya hivyo, alifanya kosa alipolifanya mara ya kwanza. Mnaona? Humpi mmoja kipande cha ugali na huyo mwingine kipande cha keki. Yote ni sawa, sawa kabisa. Mnaona? Sasa, angalia, Yeye ni, Yeye—Yeye—Yeye hana kikomo, mkamilifu, mwenye nguvu zote, yuko kila mahali. Sasa, tumeona hapo ya kwamba Msamaria huyu . . . Sasa, Yeye atajitambulishaje Mwenyewe kwa Samaria? Swali liko kati Yake na huyo mwanamke.

Na baada ya kumtazama kwa dakika chache, Baba alikuwa amemtuma huko juu, kwa hiyo Yeye—Yeye akasema, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

“Loo,” Yeye akasema, “hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Kwa hiyo umesema vema.”

166 Ninaweza kuona lundo hilo kubwa la nywele za kipilipili, likishuka juu ya mabega yake, na macho yake makubwa ya hudhurungi, na machozi yanatiririka mashavuni mwake. Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Ni tofauti jinsi gani na yule kahaba, na hao wahubiri. Alikuwa amemjua Mungu sana kuliko nusu yao; ndivyo ilivyo siku hizi, pia. Hiyo ni kweli. Naam.

167 Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Akasema, “Tunajua, sisi Mas-. . . sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja, hiyo itakuwa ndiyo ishara atakayofanya. Kwa hiyo hapana shaka Wewe ni Nabii Wake. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya; lakini u Nani Wewe?”

Loo, jamani. Kamwe hapajakuwapo ila Mmoja angeweza kusema jambo hili. Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

Yeye alitambua jambo hilo. Huyo alikuwa ndiye Masihi ambaye alikuwa amefundishwa kwamba alikuwa yuaja. Alijua Yeye angekuwa ni Nabii, Mungu-Nabii. Kwa hiyo akasema . . .

168 Akaangusha mtungi wake wa maji, ama, akauweka chini, ama nini, kisha akakimbia mjini. Basi uangalieni ujumbe wake. Akaingia mbio, kasema, “Njoni mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Je, hii si ndiyo ishara yenyewe ya Masihi? Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi? Hivi Maandiko yetu hayatwambii ya kwamba atakapokuja, hivyo ndivyo atakavyofanya?”

169 Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mji huo walimwamini Yeye kuwa ndiye Masihi kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke ambaye alikuwa amemwambia mambo aliyokuwa amefanya. Je, hayo ni Maandiko? Yohana Mtakatifu 4.

170 Sasa, ninaona wakati wangu unakwisha, kwa hiyo itanibidi kuharakisha sasa na kufanyiza mstari wa maombi. Sitaki kuwaweka muda mrefu sana. Mnaona? Lakini hii, iwe ndiyo ibada ya mwisho ya uponyaji, kadiri nijuavyo sasa, mpaka Jumapili usiku. Lakini sasa, ngojeni. Hebu nichukue maskini—maskini nyundo moja zaidi hapa kupigilia msumari hapa ndani kuufanya ushikilie.

171 Sasa, kulikuwako na Wayahudi: Yeye alijitambulishaje Mwenyewe kwa Wayahudi kama Masihi? Kwa kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii. Hiyo ni kweli? Nyote mnakubaliana na hilo? Sasa, kumbukeni, walio Wake, walio Wake. Hao Wayahudi wengine, Wayahudi tu wa kawaida, hao wahudumu wa kitabaka, na makasisi wamesimama pale wakiwa na D.D.D., Ph.D., LL.D., wamesimama pale, mwajua, huku ukosi wao umepinduliwa, tuseme, wamevaa vilemba, na wote namna hiyo, walisema, “Ni—ni telepathia ya kiakili. Msininii . . . Mnaona? Angalieni tabaka lake. Angalieni alikotoka. Yeye ni

nini kwanza kabisa? Alitoka shule gani? Alijifunza hili wapi? Hatuna kumbukumbu yake hata akihudhuria seminari zetu, kwa hiyo mnajua hawezi kuwa sahihi. Yeye si wa Assemblies. Yeye si wa Umoja. Yeye si wa Church of God, Baptisti, Presbiteri, ama Katoliki. Hatuna kumbukumbu ya yeye kuwa katika shule zetu."

172 Ninajua ninaumiza, lakini mama yangu alizoea kuniambia. . . Tulikuwa watoto wadogo, sisi. . . ninyi. . . tuliishi—tuliishi maskini sana, huko nyuma milimani, ilitubidi ku—kuchukua ugali wa mahindi, mwajua, na kutoa mafuta kutoka kwenye maganda ya nyama ya nguruwe tungechukua, na kupika ugali wa mahindi. Na kila Jumamosi usiku ingetubidi ku—kuoga, na kunywa dozi ya mafuta ya mbarika, kusudi tujitayarishe kwa ajili ya Jumapili asubuhi, turudi shuleni. Ili—ilikuwa mbaya sana, chakula che—chetu, tungeshikwa na pellagra na kadhalika. Mboga za tanipu, na njegere zenye macho meusi, na ugali wa mahindi, na molasi ya mtama, hizo karibu ndizo tulizolelewa kwazo. Kwa hiyo ingetubidi kunywa hayo mafuta ya mbarika, naye Mama alikuwa akininii. . . Ningeanza kuyanywa, ningesema, "Loo, Mama. Tafadhali, tafadhali, yananichefua sana."

Naye angesema, "Yasipokuchefua, hayakufai kitu."

173 Kwa hiyo labda hili litachochea ulaji wenu wa kiroho mahali fulani, ambalo litawafanya wazima kabisa na kuchefukwa; hilo litawafanya watu kuyachunguza Maandiko, kwa kuwa Hayo ni ya kweli. Hayo ni Neno la Mungu. Hayo Ndiyo yasiyoweza kukosea. Hayo Ndiyo yanayomshuhudia Masihi. Amina. Yeye husimama na Neno Lake. Amina.

174 Mimi sijiitikii "amina" mwenyewe, bali *amina* linamaanisha "na iwe hivyo." Ni—ninaliamini kwa moyo wangu wote, ya kwamba mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitapita kamwe.

Angalieni, mwanamke huyu Msamaria. Ilimbidi Msamaria kutambua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Kristo.

Sasa, "Vipi kuhusu Mataifa, Ndugu Branham? Unawaacha nje."

175 Hakuna hata mahali pamoja katika Maandiko ambapo Yeye alipata kufanya ishara hiyo mbele ya Mmataifa. Patafute na unionyeshe. Hakuna. La, bwana. Hakuna. Alionyesha ishara Yake ya Masihi kwa wale waliokuwa wakimtazamia Masihi. Loo, tafadhali lishikeni hili vizuri. Hilo ndilo jambo lile lile analofanya siku hizi. Sasa, nitawaonyesha ni kwa nini.

176 Sasa, angalieni. Kabla hajaondoka, hata hivyo, alitabiri juu ya wakati wa Mataifa. Sasa, Wayahudi, walikuwa na miaka elfu nne ya kumwamini Masihi, na Wasamaria kutoka huko nyuma kabisa katika wakati wa Musa, wakati walipowaoa hawa wanawake wa Moabu, na kadhalika, na kuvunjika-vunjika na kuwa nusu machotara, na kadhalika. Sasa, wote walikuwa na

miaka hii yote ya kumtazamia Masihi, na kulikuwako na baadhi ya *wenye-mioyo-myeupe* mle ndani, sasa angalieni: Walio Wake.

Hebu semeni pamoja nami, "Walio Wake."

177 Alijitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake, sasa angalieni, wengi wa Wayahudi hawakumwamini. Kwa sababu tu walikuwa Wayahudi, hilo halikuwa kitu, ila wale ambao majina yao yalikuwa yameandikwa katika Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

178 Mnakumbuka, Biblia ilisema ya kwamba wote, mpinga-Kristo katika siku za mwisho, ambaye alikuwa ni madhehebu ya kidini. . . Nitalifikia hilo juma hili, Bwana akipenda, ama juma lijalo, mnaona (vema), na kuthibitisha ni mpinga-Kristo. Biblia inasema hivyo. Hiyo ni kweli. "Naye aliwadanganya wote wakaao juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hapo ndipo ilipokuwa. Mnaona?

179 Sasa, hao ambao, "Wote alionipa Baba (wakati uliopita) watakuja Kwangu. Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Si kwa sababu ya ukoo ama jamii, bali, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Sasa, angalieni.

180 Sasa, mnasema huo ni Ukalvini. Mimi si Mkalvini sasa. Ninaamini ya kwamba usalama unaambatana na Kanisa. Kweli kabisa. Lakini kama uko Kanisani, umefanywa salama pamoja nalo. Lakini je, uko Kanisani, ndilo jambo linalofuata? Sasa, jambo ndilo hilo. Si kwa sababu unasema ndivyo ulivyo, hilo halikuweki humo.

181 Sasa, lakini, angalia, ndugu, tukiliacha somo hilo, tunarudi kwa mwanamke Msamaria. Sasa, angalieni yale aliyosema pale. Sasa, alisema, "Mbona, bila shaka. Tunajua huyo ni Masihi. Atafanya ishara hiyo atakapokuja."

182 Sasa, kabla Yesu hajaondoka, katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Mliwahi kusikia hilo? Sasa, hebu. . . Yeye alisema kwanza, kuhusu wakati wa Nuhu, alisema ule wa Nuhu: kula, kunywa, kuoa, kuolewa.

183 Lakini huko Sodoma, sasa, hebu tuangalie. Sasa, daima kuna matabaka matatu ya watu. Waangalie kwa makini. Sasa, Sodoma iliwakilisha hasa matabaka matatu ya watu, kama ilivyokuwa wakati wa Nuhu, wakati ulimwengu ulipoangamizwa kwa maji. Sasa, huko Sodoma iliangamizwa kwa moto. Hiyo ni kweli? Sasa, angalieni. Kulikuwa na matabaka matatu ya watu na Wajumbe watatu. Sasa, Ibrahimu aliwakilisha "Walio Wake."

Liseme tena: "Walio Wake."

Ibrahimu na kundi lake walikuwa nje ya Sodoma, nalo neno lenyewe *kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke, waliotengwa."

184 Lutu alichukua chaguo lake na madhehebu yake, kisha akashuka akaenda kule, akawa meya wa jiji hilo. Naye mke wake alikuwa ni mfuasi wa shirika lote, naye alivaa mtindo wa Hollywood, na kadhalika. Mnaona kilichompata? Yeye angali amesimama pale kama nguzo ya chumvi. Sasa, lakini huko alitamani kuwa Hollywood. Mnaona? Alitaka kuwa kama walimwengu wengine.

185 Lakini Sara alikuwa ndiye mwanamke mrembo kuliko wote ulimwenguni, naye akachukua chaguo lake pamoja na mumewe na kuishi huko nje kwenye nchi kame, ili aweze kumtumikia Mungu na awe mrithi wa ile ahadi. Ni tofauti jinsi gani.

186 Sasa, mambo yalipokuwa magumu, si mambo mazuri, makubwa mno, bali yanakuwa magumu: Siku moja Ibrahimu alikuwa ameketi kwenye kivuli cha mwaloni, naye akaangalia huko nje, hapana shaka ilikuwa yapata adhuhuri, naye akawaona Watu watatu wakija, wamejaa mavumbi juu ya nguo Zao. Sasa, shikilieni hayo Maandiko mawili, sasa. Sasa, aliwaona, wamejaa mavumbi nguoni Mwao. Nao wakamkaribia. Naye Ibrahimu, akiwa wa kiroho na akingojea kuiona ahadi ile, upesi (Yeye alikuwa "aliyeitwa atoke.") aliitambua. Kulikuwa na jambo la kigeni kuhusu hao Watu.

Loo, bila shaka huenda walisema, "U hali gani, bwana? Sisi ni Wageni. Tumetoka nchi ya kigeni."

187 Akaenda kuwalaki, kasema, "Njoni huku mkaketi chini ya mti. Ningependa kuzungumza Nawe kwa dakika moja tu. Hebu nilete maji kidogo mkanawe miguu, nikawape chakula kidogo, kisha mwendelee. Ketini chini. Hiyo ndiyo sababu mmekuja, Mungu aliwatuma huku ili niweze—niweze kuwafanyia hivi."

"Vema," Wakasema, "nenda, na iwe hivyo," basi wakaenda, wakaketi chini.

188 Ninaweza kumwona akiingia hima, kasema, "Sara," huko nyuma kabisa hemani, kasema, "kanda unga kidogo. Chukua kipepeta, na upepete unga kidogo hapa, ama chochote kile, ndipo uoke keki kwenye makaa." Ndipo akatoka akamchukua ndama mdogo aliyenona, akamchinja, na kumpa mtumishi, kasema, "Mtengeneze."

Naye akamtengeneza vizuri, na kumleta mbele Zake, akaketi chini. Sasa, angalieni.

189 Kama ilivyokuwa katika Sodoma, itakuwa hivi, kwa sababu huu ndio wakati wa kuteketezwa. Mnaamini hilo? Afadhali mwamini jambo hilo, wakati haidrojeni, na mabomu ya atomiki, na sputniki, na kadhalika yakiruka kote karibu nanyi, afadhali uwe ukiamini, kwa sababu yanakuja.

190 Angalieni. Sasa, ni kitu gani kilichotukia? Haya hapa yaliyotukia. Hao Malaika waliketi pale kidogo, Hao watatu. Waliendelea kuangalia upande wa Sodoma. Baada ya kitambo kidogo. . . Sasa, kumbukeni, wawili wao walishuka kwenda Sodoma. Ni wangapi wanaojua hilo? Wawili wao walishuka kwenda Sodoma, nao wakahubiri. Loo, Billy Graham ma—mamboleo, mnaona, alishuka akaenda Sodoma, kwa sababu kulikuwa na. . . Lutu alikuwa kule chini, ambaye aliwakilisha mwaminio vuguvugu, mwaminio mkwamia mpakani, ndugu wa kidhehebu. Alikuwa huko chini Sodoma pamoja na walimwengu wengine. Kusanyiko lake lote lilikuwa la kilimwengu na kadhalika. Lakini alikuwa huko chini.

191 Nao wakamtuma Billy Graham wa kisasa huko chini na kuwahubiria, hakuna miujiza, ila tu aliwapofusha; na kuhubiriwa kwa Injili kweli humpofusha asiyeamini. Tunajua hilo. Si—si—si Lutu aliyepofushwa, bali, walipofushwa, hasa, bali hao wengine walipofushwa.

192 Sasa. Lakini sasa, tunaona ni ishara ya namna gani waliyofanya: walihubiri Injili kwa njia ambayo ilimpofusha asiyeamini hasa na kumwita Lutu atoke kabla moto haujashuka. Hiyo ni kweli?

193 Mwangalieni Jamaa huyu, alibaki nyuma, alilipa Kanisa ishara gani, "Walio Wake." Yule aliyebaki nyuma hakuwa Malaika, alikuwa ni Mungu. Biblia ilisema alikuwa ni Mungu, Ibrahimu alimwita *Elohimu*, yule Ajitoshelezaye kwa Yote, herufi kubwa B-w-a-n-a. Alipaswa kujua, yeye ndiye aliyekuwa akizungumza Naye. Mungu. . .

Mhudumu mmoja aliniambia wakati—wakati mmoja, akasema—kasema, "Unamaanisha huyo alikuwa ni Yehova Mungu?"

Nikasema, "Huyo alikuwa Yehova Mungu. Loo," nikasema, "unashindwa tu kujua jinsi Yeye alivyo mkuu."

194 Tumeumbwa na nini? Elementi kumi na sita: kalisi, potashi, petroli, nurulimwengu. Alichukua tu konzi moja na kufanya "Whiu! Njoo hapa, Gabrieli, ingia kwenye huu." Mnaona? "Whiu!" Akapuliza moja hapa kwa ajili ya Malaika mwingine. "Whiu!" Akapuliza kwa ajili yake Mwenyewe. Wakashuka moja kwa moja, wakala nyama ya ndama, wakanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, wakala ugali, kisha wakatoweka papo hapo mbele ya Ibrahimu. Mnaona?

195 Vema, huyo ndiye Mungu anayetumiliki. Huenda nisiwe kijiko kimoja cha majivu, wala wewe pia, bali Yeye anaweza kunena (Haleluya!), nitatokea. Ataniita. Nina furaha kwamba Yeye ananijua, nami nina furaha kwamba ninamjua. Yeye ni Yehova. Huyo hapo. Alikuwa akiwakilisha nini? Kile angekuwa katika siku za mwisho, akiishi katika mwili.

196 Sasa, angalieni kwa makini. Sasa, tunaona ya kwamba ni. . .Hebu tuone ni ishara ya namna gani aliyowapa walio Wake. Kama vile alivyofanya wakati alipokuja duniani, Mungu aliyefanyika mwili katika Kristo. Sasa, angalieni, Yeye alikuwa amegeuza mgongo Wake. Naye akasema, "Ibrahimu (Alijuaje alikuwa ni Ibrahimu?), yu wapi Sara, mkeo?" Ati nini? Alijua jina lake lilikuwa Ibrahimu, alijua ya kwamba alikuwa ameoa, na alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa Sara.

Ibrahimu alishangaa sana, akasema, nayo Biblia inasema hasa Ibrahimu alisema, "Yuko hemani nyuma Yako."

197 Wanawake hawakutenda wakati huo kama wanavyofanya sasa: kurandaranda, na kuwa, kupachukua mahali pa waume zao, na kushughulikia biashara zote, na kupiga kura katika siasa, na kuwaingiza jamaa kama yule ndio kwanza wamwingize, na mambo kama hayo. La. Hawakufanya hivyo wakati huo. La. Walijua zaidi kumhusu Mungu. Sara alimwita Ibrahimu bwana wake.

Sasa, kasema, "Yuko hemani nyuma Yako." Hemani nyuma Yako.

198 Akasema, "Ibrahimu," (Sikilizeni!) "Mimi," (Loo, rehema! *Mimi*, hicho kiwakilishi nafsi tena.) "Katika muhula wake nitakurudia, kama nilivyokupa ahadi hiyo hapo mwanzoni, miaka ishirini na mitano iliyopita."

199 Huyu hapa Mtu akila ugali, akila nyama ya ndama, na kunywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, pamoja na siagi kwenye mkate, hapana shaka, ameketi pale akila huo, na kusema, "Nilikutolea ahadi, nami nitaitimiza." Amina.

Naye Ibrahimu akamwita *Elohimu*, Mungu Mwenyezi. Hapo, alikuwa, ameketi pale, kasema, "Nitakurudia katika. . . "

200 Naye Sara, huko nyuma kwenye hema, akafanya, akacheka, kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe hapa, mwenye umri wa miaka mia moja, ati nipate raha na bwana wangu tena namna hiyo? Loo, isingewezekana."

201 Naye yu—yule Mtu aliyeketi pale akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Loo, ni telepathia ya namna gani hiyo? Ni ninii ya aina gani. . .? Yule mwanamke hemani nyuma Yake. Kasema, "Kwa nini akacheka?"

202 Sasa angalieni, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," kwamba Mungu angejidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa kibinadamu, Kanisa Lake, Mwili wa Kristo, naye angefanya ishara ile ile. Hapo Mataifa wanalipata.

203 Sasa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaona jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi? jinsi alivyojitambulisha kwa Mataifa? na, ama, kwa Wasamaria? na kuwaahidi Mataifa.

204 Sasa, tumekuwa na miaka elfu mbili, halijawahi kuwa kanisani. Lakini itakuwa Nuru wakati wa jioni. Nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa usiku wala mchana, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru."

Sasa, sikilizeni. Hebu ni . . . Siku moja juma hili, Bwana akipenda, ninataka kuhubiri juu ya *Wakati Mashariki Na Magharibi Zinapokutana*.

205 Sasa, kila mtu aliye na elimu yoyote anajua ya kwamba ustaarabu umesafiri pamoja na jua, kutoka mashariki hadi magharibi. Ni wangapi wanaojua hilo? Bila shaka mnajua hilo. Ustaarabu, ulio wa kale sana tulio nao ni Uchina, nasi tunakuja moja kwa moja. Ustaarabu umesafiri pamoja na jua.

206 Sasa, katika watu wa mashariki . . . Kwenye upeo wa macho wa mashariki j-u-a huchomoza na kutua magharibi, kwa watu wa magharibi: j-u-a. Na M-w-a-n-a wa Mungu, sawa na j-u-a la Mungu, M-w-a-n-a wa Mungu alikuja kwa watu wa mashariki kwanza, Wayahudi, na kwa hiyo . . . Hiyo ni kweli? Wayunani na kadhalika, alikuja mashariki.

207 Sasa, kumekuwa na miaka elfu mbili ambayo imekuwa ya utusitusi. Wameunda madhehebu, na kujenga hospitali, na wakajenga makanisa, wakafanya tu yale Yesu aliyowaambia wasifanye. Kamwe hakusema tujenge makanisa. Kamwe hakusema tujenge madhehebu. Kasema, "Hubirini Injili (Hiyo ni kweli.), dhihirisheni nguvu za Mungu."

208 Lakini mambo haya yamechukua mahali pake. Yameishia siku zao. Lakini sasa, "Wakati wa jioni," Yeye alisema, "itakuwa Nuru." Naye Mwana yeye yule aliyeangazia mashariki anaangazia magharibi. Ishara zile zile za Masihi zilizofanywa kule kuthibitisha alikuwa ni Masihi, zinaangazia magharibi. Nasi tuko kwenye Pwani ya Magharibi. Tuko yadi mia tano, karibu, kutoka baharini. Na kama tukienda hivyo, tunaenda wapi? Kurudi Uchina tena. Mashariki na magharibi zimekutana.

209 Hiyo ndiyo sababu dhambi inalundikana hapa kwenye Pwani hii ya Magharibi. Ni mbaya sana, na ni ovu. Mbona, tulikuwa tukiagizia huko Ufaransa tupate mitindo. Ufaransa huagizia kwetu wapate mitindo kutoka kwa hawa wanawake.

210 Wanawake wetu wa Kipentekoste, hamna aibu. Ninyi wanaume wa Kipentekoste, mnaovuta sigara na kufanya yasiyofaa, na kuoa wake watatu ama wanne, na ni mashemasi makanisani. Jioneni aibu. Mungu na azirehemu nafsi zenu zenye dhambi. Nanyi madhehebu ya—ya Methodisti, na Baptisti, na Assemblies of God, na Churches of God yanayoruhusu hilo . . .

211 Unasema, "Daima unawakemea wanawake." Mwanamume yeyote atakayemruhusu mke wake kuvaa kaptura na kuvuta sigara, inaonyesha ameumbwa kwa kitu gani. Yeye si mwanaume.

"Loo," mnasema, "wewe ni—wewe ni katili, Ndugu Branham."

212 Sivyo. Mimi si katili. Ninahubiri Neno la Mungu. Ni kweli kabisa. Jioneni aibu. Jitikiseni mkarudie fahamu zenu. Mrudieni Mungu. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Mabwana, tunataka kumwona Yesu.

213 Je, alizembea? Kuna nabii yeyote aliyewahi kuzembea? Yeye alitia muhuri ushuhuda Wake kwa Damu Yake. Watu wa kweli wa Mungu kamwe hawatakivumilia kipindi cha televisheni mahali fulani, ama kuingiza pesa humo, ama mradi fulani mkubwa wa elimu. Atasema kweli. Kama itamgharimu uhai, atasema ukweli. Hiyo ni kweli.

214 Huenda wakakuchukia siku moja, lakini siku nyingine yaja ambapo watakupenda, maana unasema kweli. Neno la Mungu linasema ni kweli. Hakuna Andiko katika Biblia kwa ajili ya matendo ya kanisa la Kipentekoste siku hizi, hata kidogo, ni kinyume chake, sembuse ninyi Wabatisti na Wamethodisti.

215 Whiu! Ninajua hilo ni kali, lakini hivyo ndivyo ninavyotaka liwe, kusudi mpate kulainika. Na siku moja mtakutana huko kwenye Kiti cha Hukumu. Ndugu, ni Neno la Mungu. Wachungaji wenu na kadhalika, wamekuwa dhaifu kuliko maji ya kuoshea vyombo. Ni, kanisa ni riziki badala ya mimbara. Hiyo ni kweli.

216 Tunahitaji watu wa Mungu watakaosimama na kusema kweli, haidhuru inamwudhi nani. Kama inahitaji mashemasi, wadhamini, na chochote kile, iweni waaminifu.

217 Mteteeni Mungu, na mwamini Neno Lake, naye Mungu atalithibitisha Neno hilo. Lililenga shabaha wakati mmoja; litailenga tena. Lakini huna budi kuilenga pamoja nalo. Huwezi kushikilia mtutu wa bunduki *hivi* na kutarajia kupiga upande *ule*. Hutapiga. Ishikilie kushoto na kulia. Haitafanya hivyo. Itapiga mstari ulionyoka. Hatuna budi kuingia katika Maandiko haya na kuifyatua moja kwa moja. Amina.

"Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, hata milele."

Tupeni dakika kumi na tano, sivyo? Roho Mtakatifu kanisani hapa.

218 Sasa, kama nimewadhuru, sama-. . . La, msinisamehe. Huh-uh. Msifanye hivyo. Nendeni tu nyumbani, wazieni jambo hilo kidogo. Sikuninii. . . simaanishi. . . Itanibidi kusema mambo wakati mwingine yanayokata kama visu na. . . Lakini—lakini, ndugu, ni—ninawajibika. Ninawajibika mbele za Mungu kusema yaliyo kweli. Ndipo kama nimesema kweli, Mungu atathibitisha kwamba ni kweli. Sasa, hebu tuone kama nilisema kweli au la. Hebu tumwombe Baba aje jukwaani. Hebu na tumwombe Mungu aje, na kuunga mkono kile. . . kama hiyo ni kweli. Kama

si kweli, Yeye hataliunga mkono. Kama ni kweli, Yeye ataliunga mkono.

219 Nanyi watu ambao mngetaka kumwona, kama atakuja na kufanya jambo lile lile usiku wa leo katika kanisa hili. . . Haidhuru atanitia mafuta kiasi gani, hana budi kukutia mafuta pia. Yesu alienda katika nchi Yake Mwenyewe, wala asingeweza kufanya miujiza mingi mikubwa kwa sababu ya kutokuamini kwao. Lakini alipompata mtu aliyemwamini, mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi Lake naye akafanywa mzima kabisa. Naam. Je, mngetaka kumwona Yesu?

220 Sasa, kama. . .Haidhuru angekuwa amevaa namna gani, jinsi angeonekana, kama Uhai huu uko ndani Yake, ndani ya mwanadamu ama watu, utafanya mambo yale yale aliyofanya, kwa sababu Yeye aliahidi jambo hilo. Je, hiyo ndiyo ishara ya Masihi sasa kwa siku za mwisho? Ni wangapi wanaufahamu vizuri? Inua mkono wako, useme, "Ninaelewa. Ninaamini hilo." Na tuombe.

221 Baba mwenye rehema, loo, kwa nini inibidi kusema mambo hayo namna hiyo? Mimi—mimi. . .Watu wanaowalisha watoto wangu, wa—watu wanaoweka nguo mgongoni mwangu, na kulipia safari zangu kote nchini, na hata hivyo, Mungu, jalia wafahamu ya kwamba ni—ninajaribu tu kuwatikisa, Bwana. Ni—ninajaribu kulirudisha kanisa kwenye njia ya kale tena. Hebu waelewe. Jalia Roho Mtakatifu awajalie kujua si katika ukatili, si katika, kutojali, bali ni kuwa mkweli, Bwana, na kusema kweli haidhuru.

222 Sasa, Baba, utaunga mkono ukweli Wako kwa ajili yetu usiku wa leo? Nimewapa tamshi kali ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jalia Roho Mtakatifu aje usiku wa leo, Baba, na kulitia mafuta kundi hili dogo la watu hapa.

223 Na wajue ya kwamba watu hawa. . .Ninasema mambo haya, lakini yanarekodiwa hapa. Kanda hii itaenda kote ulimwenguni. Itatafsiriwa katika lugha nyingi, nyingi mbalimbali kote ulimwenguni, na watu kutoka kila mahali watakuwa wakiisikia. Nami sina budi kuyapima maneno yangu, Bwana, ya kwamba ni kweli na ni Maneno Yako, wala si yangu.

224 Ninakunukuu tu Wewe, nikikiri, kama Biblia isemavyo, ya kwamba Wewe sasa ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Ninakiri Neno Lako ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nena, Bwana Mungu, na uwajalie watu wajue ya kwamba—ya kwamba ulitoa huo Ujumbe, si mtumishi Wako. Tujalie, Bwana.

225 Tunayakabidhi yote Kwako sasa. Nisingeweza kusema zaidi. Na Neno moja kutoka Kwako litakuwa zaidi ya yale mhubiri yeyote angeweza kuhubiri katika miaka milioni moja, Neno moja tu. Tunajua Liko hapo, tunajua ni kweli.

226 Na sasa tunakutaka ulithibitishe Neno kwa ishara zinazofuata, kama ulivyoahidi, wapate kujua ya kwamba nimewaambia kweli, ya kwamba Wewe ndiwe Masihi. Nguzo hii kuu ya Moto waliyo na picha yake, hapa, na kutoka Ujerumani, kutoka Uswisi, kutoka kote nchini, ambako wameipigia, kwamba ni Nguzo ile ile ya Moto iliyoambatana na wana wa Israeli.

227 Wakati alipokuja hapa duniani, tunaona ya kwamba Nguzo hiyo ya Moto ilikaa katika mwili, Mwana wa Mungu. Tuliangalia kazi alizofanya. Akasema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu." Baadaye, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka Yeye alirudi kwa Baba.

228 Basi siku moja Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski kuwakamata watu, na Nguzo iyo hiyo kubwa ya Moto ikamwangusha chini, Nuru iliyoyapofusha macho yake, ikamfanya kipofu kwa muda.

Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Hakujua hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni nini. Akasema, "U nani Wewe?"

"Ni vigumu kwako kupiga teke michokoo."

"U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu."

229 Sasa, Bwana, ulimwengu wa kisayansi unajua, baada ya wao kupiga picha, kwamba ni Nguzo ile ile ya Moto. Ni Nuru ya kisiri ambayo si ya ajabu tu, bali imepigwa katika lenzi ya kamera kote ulimwenguni.

230 Sasa, kama ni Roho yeye yule, basi atafanya kazi ile ile kama watu wanaweza kujiweka katika hali ile ile. Jalia iwe usiku wa leo, Bwana, ambapo mimi na kanisa hili, na hawa ndugu, upate kujithibitisha Mwenyewe kwamba ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

231 Tutakapoondoka usiku wa leo tutaninii, kama wale waliotoka Emau, tunataka kukuona ukifanya sasa, mambo uliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, na ahadi Zako kwamba ungefanya hivyo, na baada ya miaka elfu mbili, naomba ujidhihirishe Mwenyewe usiku wa leo, na tutakapoenda nyumbani, tutasema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipojitambulisha Mwenyewe miongoni mwetu usiku wa leo?"

232 Na Bwana, ninaamini itawafanya watu warudi kwenye maombi na kufunga, na—na kanisa hili dogo litakua, na nguvu za Mungu zitakuwa ndani yake, na utabiri na ishara kuu na maajabu, huku wanawake na wanaume wakijinyosha na kutembea mbele za Mungu kwa upole. Na, loo, ni hofu ya Mungu ya jinsi gani itakayokuja nchini, Bwana. Wape ishara kuu na maajabu. Tujalie. Litie nguvu Kanisa Lako, Bwana.

233 Ee Mungu, waite watu Wako; watoe katika machafuko haya katika siku za mwisho. Tujalie. Tutakungojea, Baba, unene nasi katika mstari wa maombi, tunapoita, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

Sasa, kama mtatuvumilia tu kwa ninii chache. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

234 Mlipata kuiona lini ikishindwa? Haishindwi, kwa sababu ni Mungu. Haiwezi kushindwa. Mungu ameituma hiyo. Na ni halisi tu kwangu kadiri ilivyo kwenu kunywa maji. Mnaona? Nina hakika tu ya kwamba Mungu atajitokeza jukwaani kama ninavyosimama kwenye jukwaa hili usiku wa leo, kwa sababu ni ahadi Yake.

235 Na kama atafanya hivyo, basi hilo litaonyesha ya kwamba Yeye ni Masihi yeye yule akirudi. Sasa, kwa akina nani? Si kwa watu wa nje, yale madhehebu makubwa na kadhalika, bali kwa Wateule (Mnaona?), kwa Kanisa. Mnaona ninalomaanisha? Walio Wake.

Mnasema, "Kwa nini usiwe na kipindi kikubwa mno cha televisheni?"

Alituma kwa walio Wake, Wateule, walioitwa watoke, si kwa madoido.

236 Yesu hakuwa na maonyesho. Hakuwa mtu wa maonyesho. Yeye—Yeye. . . Wao walisema, "Kwa nini usiondoke kwenye kundi hilo huko chini mtoni? Unajipumbaza na kundi linaloonekana tu kama la watakatifu wanaojibingirisha," mwajua. "Njoo huku juu ukamwonyeshe Kayafa yale unayoweza kufanya." Kamwe hakufanya hivyo. Uh-huh. Alikuwa, alikaa kwa unyenyekevu, kwa utulivu.

237 Alikuja kwa walio Wake, kuninii. . . Alijitambulisha Mwenyewe kwa walio Wake, mbele ya Wayahudi, hao waliomkataa, walikwenda Umilele. Wale waliompokea na kuliamini, jina lao halipatikani na mauti, nalo litakuwa la milele. Hiyo ni kweli.

238 Sasa, mimi si Yeye. Mimi ni ndugu yenu tu. Mimi ni ndugu yenu, mtumishi wa Yesu Kristo, nimetumwa hapa pamoja na ndugu zangu, na pamoja nanyi watu hapa, kuninii. . . pamoja na karama inayodhihirisha. Na kama ningalikuwa na wakati, ningeweza kuipitisha kote katika Biblia juma hili, na kuwathibitishia kwa Andiko baada ya Andiko, mathibitisho yasiyoweza kukosea ya kwamba hii ndiyo saa yake. Msiache liwapite. Mnaona?

239 Huyu hapa msichana. Sijawahi kumwona maishani mwangu, msichana mzuri. Huenda akawa ni Mkristo; huenda asiwe. Huenda akawa—huenda akawa mgonjwa; huenda asiwe. Huenda akawa na matatizo ya kifedha, matatizo ya kinyumbani.

Sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini huu hapa mtazamo mkamilifu wa kile nilichokuwa nikizungumzia.

240 Hii hapa mandhari ndogo usiku wa leo. Huyu hapa mwanamume na huyu hapa mwanamke, wakikutana kwa mara yao ya kwanza. Yeye aliinua tu mkono wake, hakunijua, na hii hapa mikono yangu simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Mnaona? Naye alisema hatufahamiani. Hiyo ni kweli, mama? Sisi hapa.

241 Sasa, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Angefanya nini kama angejitokeza jukwaani? Kama tu vile alivyofanya kwenye siku ile kisimani, yule mwanamke Msamaria. Hiyo ni kweli?

242 Sasa, Yeye anaweza kufanya nini? Ni kunitia mafuta na kumtia mafuta. Asipofanya hivyo, siwezi kusema jambo moja. Hii ni bubu kiziwi mpaka kitu fulani kinene ndani yake. [Ndugu Branham aliigonga maikrofoni—Mh.] Nami pia. Simjui. Yeye hanijui. Kwa hiyo ni—nitajuaje lolote kumhusu?

Sasa, vipi kama ningesema, "Mama, wewe ni mgonjwa?"

Angesema, "Naam, bwana, Bw. Branham, mimi ni mgonjwa."

243 "Utukufu kwa Mungu! Haleluya!" Nimtikise, niseme, "Utukufu kwa Mungu! Upokee. Haleluya! Endelea. Umeponywa." Hiyo inaweza kuwa sawa. Hakika, hilo lingekuwa sawa. Angeliamini, angepona. Bila shaka.

244 Kama tu vile Charlie Fuller alivyosema hapa chini wakati mmoja, Ndugu Fuller, akasema, "Ninaamini katika karama hizi, pia ninaamini katika karama hizi kuu za uponyaji pia, lakini," kasema, "hizo ni karama za uponyaji, bali Mungu atawafanya watu hao wawajibike kwenye Kiti cha Hukumu kwa kuifanyia biashara." Nami ninaamini hivyo pia. Amesema kweli, hapo. Naam, bwana. Usimfanyie Mungu biashara. Hawezi kufanyiwa biashara. Lakini Mungu atakufanya ulipie kile unachofanya, jinsi unavyokitumia.

245 Sasa, mama, hatufahamiani. Mtu fulani, ana kadi ya maombi mkononi mwake, mtu fulani anapaswa kuichukua. Njoo hapa, Mpendwa. [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo, ni—loo, si—sivyo, sawa, ni kitu kingine hapo, kitu kingine pale. Nilifikiri ilikuwa ni kadi ya maombi. Samahani. Loo, yeye ni . . . ni kwa . . . ana kadi ya mtu mwingine. Vema.

246 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele . . . Sasa, ninawapa picha ya Biblia, kanisa la Kipentekoste, ninamaanisha *hili*, *hapa*, ninawapa picha ya Biblia na kile Yesu alichokuwa jana. Sasa, Yeye alisema ya kwamba katika siku hii ya mwisho angeshuka katika mwili wa kibinadamu, kama alivyofanya huko Sodoma, na angefanya jambo lile lile. Sasa, kama Yeye atarudi na kufanya kama

tu alivyowafanyia Wasamaria na Wayahudi, utamwamini Yeye kuwa ndiye Masihi aliye hapa jengoni usiku wa leo? Inueni mikono yenu kama mkisema, “Kama atafanya jambo lile lile, nitamwamini.”

Vema, kisa hiki kimoja kinapaswa kulitatua. Kama wewe ni mwaminifu moyoni mwako, linapaswa kutatuliwa.

247 Sasa, sisi hapa, sote wawili chini ya kiapo ya kwamba hatufahamiani. Vema. Sasa, kama Mungu atanifunulia jambo fulani ambalo umefanya, ambalo unajua nisingejua lolote kulihusu, ama jambo fulani ambalo—ambalo unapanga kufanya, ambalo sijui lolote kulihusu, ama jambo fulani kukuhusu, shida yako ni nini, ugonjwa wako ni upi, mateso yako, ama—ama *kitu kama hicho*, kitu kama hicho, basi ungeamini ya kwamba ilikuwa ni Yeye?

248 Hilo lingeninii. . .itabidi lije kupitia nguvu fulani. Kama unaamini ya kwamba ni nguvu Zake, basi unapata baraka Zake. Kama unaamini ni nguvu zingine, vema, hiyo ni kati yako na Mungu. Unaona? Nisingejua nini kingetukia hapo.

249 Sasa, kama atafanya hivyo, utalikubali, kama angelifanya kwa mtindo ule ule aliofanya katika Biblia, kama vile Yeye na yule mwanamke aliyesimama, wakizungumza, ungeamini, sivyo, mama? Nalo kanisa lilisema wangeamini. Sasa—sasa ni wakati wa Mungu kutenda kazi. Unaona?

250 Sasa, sisi hapa, labda watu mia tatu ama mia nne, mia tatu, kwa vyovyote vile, wameketi hapa usiku wa leo. Vema. Angalieni hapa, mbele ya watu mia tatu, nami nililiona mbele ya laki tano huko Bombay, India, mnaona, mia mbili sabini na tano elfu huko Durban, Afrika Kusini. Halishindwi. Ni Mungu.

251 Sasa, kama anaweza kukwambia kile umekuwa, hakika Yeye anaweza. . .ungeamini, utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Atakaponena, utajua kama ni kweli.

252 Vema, kama ndivyo, Naye akwambie kile umekuwa, vipi kuhusu kile utakachokuwa? Ungeweza kuamini hilo kwa urahisi basi, sivyo, kama Yeye angesema hilo? Vema.

253 Kijana mwanamke, sasa, sijawahi kuona maishani mwangu. Yeye ni mdogo sana kuliko mimi, tumeachana kwa miaka mingi kwa kuzaliwa, labda umbali wa maili kadhaa, na ni mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini sasa, ninazungumza tu naye kusudi niishike roho yake, kama tu Bwana wetu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Nami naona sasa ya kwamba yeye ni mwaminio, nawe unateseka. Unataka maombi kwa ajili ya namna fulani ya ugonjwa wa ngozi ulio nao. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini?

254 Sasa, ninaendelea, kila mkutano, ninahisi hilo, mtu fulani alisema, “Alibahatisha hilo.” Sasa, huwezi kuficha mawazo yako

sasa. Yuko hapa. Uh-huh. Unaona? Unasema . . . Sasa, wewe . . . Sikubahatisha hilo. Tafuta kujua.

255 Unaonekana kuwa na uhusiano mzuri na Roho wa Mungu. Sasa, sijui nilichokwambia. Huyo hakuwa ni mimi. Huyo alikuwa ni Yeye. Liko kwenye kinasa sauti pale. Ningeweza kuirudisha nyuma na kujua ilikuwa ni nini, bali sijui sasa.

Lakini kama tu utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake! (Jina hilo huwakwaza watu, mnaona.) Kwa hiyo, laiti ungeamini kwa moyo wako wote!

256 Naam, bwana, ni ugonjwa wa ngozi. Hivyo ndivyo nilivyokwambia. Na—na hili hapa jambo lingine. Unaumwa na kichwa, maumivu makali sana ya kichwa. Halafu basi, kuna watoto wawili ninaowaona ambao unataka waombewe. Na mwenye umri mkubwa kuliko wote anaugua ugonjwa wa mishipa. Yule mdogo ana tatizo la nyonga, ni uvimbe kwenye nyonga. Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, ingekufanya uamini sasa kwa moyo wako wote? Unajua sikujui, lakini Bibi Bowman, unaweza kwenda nyumbani. Mwamini Bwana Yesu Kristo na upate afya. Mungu akubariki, dada yangu.

257 Unaamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Sasa, aminini tu. Sasa, huyu hapa mwanamume. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Yeye labda ana umri mkubwa kidogo kuliko wangu. Hatufahamiani. Wala sikujui, nawe hunijui. Lakini kama Mungu anaweza kuniambia jambo fulani, ama . . .

258 Sasa, tulieni kabisa. Mtu yeyote asisogee huku na huku. Mnaona, ninyi ni roho. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho. Mnajua hilo? Huu ni mkono wangu, kama nilivyosema jana usiku, huu ni mkono wangu; hiki ni kidole changu; hili ni sikio langu; hii ni pua yangu, macho yangu. Lakini mimi ni nani? Mnaona, hicho ni kitu ambacho ni changu. Mimi ni roho.

259 Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Wewe huko kwa ajili yako mwenyewe. Mtu ambaye uko hapa kwa ajili yake ni mahututi sana. Wana uvuli wa mauti juu yao. Ni kansa. Hawako hapa. Wako Phoenix, Arizona. Nenda, amini, nao watapata afya. Vema. Kama ulivyoamini, na iwe kwako. Mungu akubariki.

Amini tu. Usiwe na shaka. Unaamini?

260 Vipi kukuhusu wewe uliyeketi hapo, mama, kitini? Ndiyo kwanza kikuchangamshe, kitu fulani kilikuchangamsha, papo hapo, sivyo? Mama huyu aliyeketi hapa na koti lake, amelala ameinua mkono wake juu, akiniangalia namna *hiyo*. Naam, papa hapa mwishoni. Unaamini shinikizo hilo kuu la damu litakuacha na utakuwa mzima? Vema, basi. Endelea tu. Unaweza kuponywa.

Aligusa nini? Yuko futi thelathini kutoka kwangu. Alimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Huyo ni Yeye.

261 Hatufahamiani, bwana. Sikujui. Huninii, labda, hunijui, isipokuwa tu kwa jina, ama kuketi mkutanoni mahali fulani na kuniona. Ni, bali kufahamiana sisi kwa sisi, hatufahamiani. Hatufahamiani.

262 Sasa, kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo unajua kwamba silijui, utamwamini Yeye kama Masihi? Si mimi, bali Yeye akifanya kazi kupitia kwangu. Ninaninii tu, karama, kujisalimisha tu kwa Roho Wake, nami nimeondoka Naye ndiye anayezungumza. Unaona? Vema, kama Yeye atakwambia, utajua kama ni kweli ama si kweli, sivyo? Unaugua, kuna kasoro kwenye mishipa. Ni mishipa iliyovimba. Hiyo ni kweli kabisa.

263 Lakini ninamwona mwanamke akitokea, mtu fulani unayemwombea. Ni dada yako. Amerukwa na akili, nawe unamwombea. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unamwamini Bwana Yesu sasa? Nenda, pokea ulichoomba.

Katika Jina la Bwana Yesu, tujalie.

264 U hali gani? Samahani. Sikuwa kwa naf-. . .kujisahau, nilikuwa nikiiangalia ile Nuru. Sikuwa na hakika. Ninaona mahali iliposimama, bali sikuwa na hakika ni nini—ni nini kilichotukia. Mnaona? Mnaona, i—inanibidi tu kuifuata. Mnaona, mimi . . .

265 Sasa, uko tayari kwa ajili ya upasuaji. Lakini unaamini ya kwamba Mungu angeweza kukuponya huo? Una vivimbe vitatu katika sehemu tatu mbalimbali. Kama nikizielezea kwako, itakusaidia? Mmoja uko kooni, mmoja uko kwenye tezi ya kike, na huo mwingine uko chini ya mkono wako wa kulia. Bibi Macintosh, hilo ndilo jina lako, nenda nyumbani na umwamini Bwana Yesu Kristo na upate afya, katika Jina la Bwana Yesu.

266 Unaamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Vema, huyo ni Yeye, ni hisia hiyo. Sasa, hivi hilo halithibitishi ya kwamba kanisa la Kipentekoste linalohisi baraka hizo, huyo ni Bwana Yesu, mnaona? Anafanya kazi zile zile. Huyo si mimi.

267 Siwajui watu hawa. Mungu Mbinguni anajua hilo. Siwajui watu hawa, lakini Mungu anawajua. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.

268 Mwanamke fulani ana leso yake kule juu. Nuru hiyo ingali juu ya huyo mwanamke. Huyo ndiye mwanamke, aliyekuwa jukwaani sasa hivi, ameinua leso yake? Ulikuwa hapa juu?

269 La, i—iko moja kwa moja nyuma yako. Huyo Mama aliye papo hapo nyuma yako ana yabisi kavu, aliyeketi hapo mwisho, mwamini Bwa-. . .hivyo ndivyo ilivyo, dada. Amina. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini hiyo yabisi kavu itakuacha? Unaamini? Kama ulikuwa na yabisi kavu, tikisa mkono wako namna *hii* ili watu wajue. Ulikuwa umeketi hapo ukiamini,

ndipo mwanamke huyo akaja na upako. Sasa, nenda nyumbani ukapate afya. Yesu Kristo alikuponya. Aligusa nini?

Sikujui wewe. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli, waweza kuinua mikono yako pamoja nami?

270 Loo, laiti watu. . . Kama ungeamini tu, ingekuwaje sasa hivi! Kungekuwa na uamsho utakaotokea kwenye Pwani hii ya Magharibi ambao ungeenea kote ulimwenguni. Laiti mngalitambua kile ninachoangalia! Na—natumaini, hakika, ni—nimepata kibali machoni penu mbele za Mungu. Ninawaambia kweli, naye Mungu anaithibitisha kwamba ni kweli. Yale Mungu anayotaka kufanya papa hapa katika kanisa hili usiku wa leo! Ni ajabu sana. Lakini ni—ninadhoofika. Mnaona? Angalia tu mkononi mwangu. Unaona jasho hili? Hiyo ni ninii tu. . . Ni wangapi wanaojua kwamba hilo linakudhoofisha?

271 Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Yeye alisema nguvu zilimtoka, Naye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Sasa, mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Danieli aliona ono moja; akasumbuliwa kichwani mwake siku nyingi. Mnaona? Aminini tu.

272 Sasa, mtu huyu, sote wawili tunasema ya kwamba hatufahamiani, hatufahamiani. Lakini Mungu anatujua. Sasa, kama anaweza kunifunulia jambo fulani kukuhusu wewe, ambalo—ambalo unajua kwamba sijui, je, lingeridhisha kwamba wewe ni. . .? Hivi ninyi wengine, hata mstari wa maombi, kila mahali, mwaweza kuamini kwa moyo wenu wote?

273 Biblia hii iliyo hapa, na mimi na mtu huyu tumesimama hapa, hatujawahi kukutana hapo kabla maishani, huku tumeinua mikono yetu, hatujawahi kukutana hapo kabla. Sasa, Yesu alisema alitambua mawazo yao. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Nalo pia ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo, makusudi na mawazo ya moyo na nia." Je, Biblia inasema hivyo?

274 Neno la Mungu, vema, Neno la Mungu lilikuwa ni nini? Yesu. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Na hapa Neno linadhihirishwa katika miili yetu. Ee Mungu! Hakika hamtalikosa, hakika, hakika. Amini.

275 Karama tu, bwana, nikijaribu kujituliza na kuishika roho yako. Kadiri linavyoweza kuonekana ni la kipekee, nimewaona wamela-. . . watu wamelala wamekufa. Ufini, sehemu tatu ama nne mbalimbali ambazo nimeona maishani mwangu, naye Mungu angeiruhusu roho yangu iondoke kwangu hata ingeingia kwenye hiyo nchi, na kuikamata roho hiyo, na kuirudisha moja kwa moja tena kwa mtu huyo. Ni kweli. Mungu Mbinguni anajua ni kweli. Mnaona? Sasa, kwa kuwa iko juu yako, nawe ungali chini ya uhuru wa kujichagulia, itakubidi kutenda. Nami

nisingeweza kufanya hivyo isipokuwa iwe ni—ni amri ya Mungu ikinionyesha ono.

Yesu alisema, "Sifanyi neno isipokuwa Baba anionyeshe."

Ndipo ungesema, "Je, anaweza kukuonyesha ya kwamba mimi ni mzima, ama kile...?"

276 Anaweza kunionyesha shida yako ni nini, bali huna budi kukubali, imani yako. Nisingeweza kukuokoa, wala nisingeweza kukuponya. Tayari limetendeka. Lakini Yeye yupo hapa sasa kuonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu yeye yule aliyeandika hayo Maneno. Mnaona?

277 Sasa. Naam, wewe ni mgonjwa sana, unajitayarisha, kwenda hospitalini kesho kwa ajili ya TB. Hiyo ni kweli. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini? Unaamini ungeweza...utapata afya, kisha uje nyumbani sasa, utakuwa mzima? Unaamini? Kama ningekwambia wewe ulikuwa nani, hilo lingekusaidia? Vema. Walter Kaiser, endelea, na uamini kwa moyo wako wote. Hiyo ni kweli. Amini kwa moyo wako wote. Kuwa tu—kuwa na imani.

278 Uliyeketi hapo, bwana, umevaa hiyo suti ya kijivu, ulikuwa na tatizo na mapafu yako pia. Kama unaweza kuamini... Naam. Unaona? Naam, alikuwa na shida ya mapafu. Niliona Nuru hiyo ikimulika juu yako, mara alipoponywa kile alichokuwa nacho pale. Alikuwa na ugonjwa wa mapafu wa namna fulani. Ilipita juu yako. Imani yako ililimaliza. Nenda nyumbani, uwe mzima. Imani yako inakufanya mzima.

279 Uliyeketi moja kwa moja nyuma ya mwanamke huyu, mwingine anayeniangalia moja kwa moja hapa sasa hivi, alikuwa na ugonjwa wa mapafu. Ni kansa, na kwenye uti wa mgongo pia. Amini kwa moyo wako wote. Maskini mama mwenye mvi, kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Simama kwa miguu yako. Mimi ni mgeni kabisa kwako. Hiyo ni kweli, punga mkono wako. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako. Vema. Ninachukua mamlaka. Unaamini hili kuwa ni kweli?

Basi katika Jina la Yesu Kristo, ninamhukumu ibilisi huyo.

Nenda na upate afya.

280 Unaamini ya kwamba ugonjwa huo wa moyo utaondoka nawe utaponywa, nawe utaenda nyumbani, kwa moyo wako wote? Basi nenda, na uamini kwa moyo wako wote, na upate afya.

281 Njoo. Unafikiri nini? Unaamini kwamba hiyo pumu itakuacha, nawe uende nyumbani, uache kukohoa? Basi nenda, amini kwa moyo wako wote, na upate afya. Kama wewe si...

282 Njoo, dada. Una wasiwasi wa nini? Umekuwa na wasiwasi kwa muda mrefu. Vema. Umeponywa sasa, nenda ukaamini kwa moyo wako wote na upate afya. Vema, bwana. Hilo ndilo linalokuvunja.

283 Vema, mama. Njoo. Unaamini kwa moyo wako wote? Ugonjwa wako wa mgongo umepona. Nenda, amini kwa moyo wako wote, na useme, "Asante, Bwana Yesu."

Moyo wenye wasiwasi, unaamini ya kwamba Yeye huuponya? Nenda, na useme, "Asante, Bwana" na uponywe. Iweni tu na imani. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya.

284 Angalia hapa, mama, niangalie. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Shida hiyo ya kina mama uliyo nayo, shida ya kike, hiyo ni kweli, nenda ukaponywe, katika Jina la Yesu.

285 Hebu kidogo. Kitu fulani kilienda kwa wasikilizaji. Naam, mtu aliyeketi papa hapa nyuma, anayeugua ugonjwa wa mgongo, akiniangalia moja kwa moja. Unaamini, bwana? Vema. Pokea uponyaji wako. Ponywa, katika Jina la Yesu Kristo. Mwaminini Mungu.

286 Mwanamke huyo aliyeketi nyuma ya huyo mwanamume hapo ana kisukari. Unaamini kwa moyo wako wote? Simama, maskini mama mwenye mvi uliyevaa miwani. Uligusa Kitu fulani, sivyo? Simama; uponywe. Nenda nyumbani, na umwamini Bwana Yesu Kristo. Amini.

287 Kama nisingekwambia kitu, nikuwekee tu mikono, ungepata...? unajua...? unaamini huyo ni Roho Mtakatifu? Njoo hapa, hebu nikuwekee mikono.

Basi, katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

288 Sasa, njoo. Waonyeshe tu jinsi wanavyoweza kufanya hilo. Mnaona? Unajua ninajua shida yako. Lakini nisiposema chochote, itakuwa sawa, nikuwekee mikono? Unaamini? Huu ni upako wa namna fulani. Amini, nao ugonjwa wako wa moyo uondoke. Alinitaka, niseme hivyo, vibaya sana.

Vema, njoo. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo, uponywe, na uende nyumbani, uwe mzima. Amini sasa, usiwe na shaka.

289 Ewe msichana, muda mfupi uliopita nilipokuwa nikihubiri, ulikuwa umeketi papo hapo nyuma ukiniangalia. Ukageuka, ukamwangalia mwanamke fulani; hisia ya kipekee sana ikapitia juu yako, wakati wewe, nilipokuwa nikihubiri, nikisema jambo fulani kumhusu Bwana Yesu, hasa sana katika siku ile nilipozungumza juu ya Sodoma, ulikuwa na hisia ya kigeni. Unakumbuka hilo? Hapo ndipo shida yako ya kike ilipoponywa. Sasa, nenda nyumbani, uwe mzima.

290 Unaamini kwa moyo wako wote? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Inueni mikono yenu. Sasa, nataka kuwaulizeni, ni wangapi wenu ni waaminio? Peaneni mikono namna *hii*. Vema.

291 Biblia ilisema hivi, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mnaamini hilo? Kama, hili, alilosema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," basi wekeaneni mikono. Usijiombee mwenyewe; mwombee mtu uliyemwekea

mikono. Wekeaneni mikono. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

292 Juu kwenye roshani kule juu, mtu huyo aliyeketi hapo akiwa na ugonjwa wa tezi dume, aliyeketi upande wa kushoto, amini kwa moyo wako wote, bwana. Jambo ndilo hilo. Mungu anakuponya, anakupa afya. Amini. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi na mwombeane sasa.

293 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunamleta Shetani kwenye shindano la kuamua. Yeye ni mdanganyifu, naye amefunuliwa usiku wa leo kwa nguvu na ufufuo wa Yesu Kristo.

Shetani, umeshindwa vita. Toka ndani ya watu hawa. Ondoka. Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yao.

294 Ninamwamuru kila mmoja wenu anayemwamini Yesu Kristo, na anajua Yeye hutimiza Neno Lake, anaamini ya kwamba huyo ni Roho Wake hapa sasa, kama unaamini kwa moyo wako wote. . . Mwaminio ameweka mikono yake juu yako, ambapo Biblia ilisema, Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Yeye ni Mungu yeye yule aliye hapa akijitambulisha Mwenyewe kwamba Yeye ndiye Masihi wenu wa Kipentekoste.

295 Kila mmoja wenu ambaye atamkubali sasa kama Mponyaji wenu, haidhuru uko wapi, simama kwa miguu yako na umkubali Yeye kama Mponyaji wako. Ninatangaza kwamba umeponywa katika Jina la Yesu Kristo. Mwinulieni mikono yenu sasa na kumsifu. Amina.

*Nitamsifu. Nitamsifu.*

Msifuni tu.

> . . . nitamsifu,
> Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
> Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,

Mungu awabariki.

61-0208 Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org